# Elimu Jumuishi

## Kitabu cha Mwalimu Tarajali

## Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali, Msingi na Elimu Maalumu



Taasisi ya Elimu Tanzania

# Yaliyomo


Orodha ya vielelezo....................iv
Shukurani....................v
Utangulizi....................vi

Sura ya Kwanza: Dhana ya elimu jumuishi....................1
Elimu jumuishi....................1
Malengo ya elimu jumuishi....................3
Misingi ya elimu jumuishi....................4
Historia ya elimu jumuishi Tanzania....................5

Sura ya Pili: Utambuzi wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu....................10
Dhana ya mahitaji maalumu....................10
Utambuzi wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji....................13
Viashiria vya mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu....................14
Mbinu za ubainishaji wa mapema kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji....................16
Zana za ubainaishaji wa mapema kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji....................17

Sura ya Tatu: Utoaji wa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu22
Dhana ya afua stahiki....................22
Umuhimu wa kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu....24
Mbinu za utoaji wa afua stahiki....................25
Afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu....................26
Changamoto katika utoaji wa afua stahiki....................31

Sura ya Nne: Mbinu na zana za ufundishaji na ujifunzaji katika mazingira jumuishi....................33
Mbinu za ujifunzaji katika darasa jumuishi....................33
Faida za kutumia mbinu za ujifunzaji katika darasa jumuishi....................34
Dhana ya zana za kufundishia na kujifunzia darasa jumuishi....................35
Aina za zana jumuishi....................35
Utengenezaji wa zana jumuishi....................37

Sura ya Tano: Mazingira ya malezi, ufundishaji na ujifunzaji katika elimu jumuishi....................39
Dhana ya mazingira jumuishi ya ujifunzaji....................39
Mbinu za uboreshaji wa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji....................41
Mbinu za uboreshaji wa mazingira ya malezi kwenye darasa jumuishi....................42
Changamoto katika kutumia mbinu za uboreshaji wa mazingira ya malezi katika darasa jumuishi....................44

Misamiati....................46
**Bibliografia**....................48


FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Kwanza

## Dhana ya elimu jumuishi

### Utangulizi

*Ufundishaji na ujifunzaji wa elimu jumuishi unahitaji ushiriki wa pamoja unaohusisha kila mwanafunzi kujifunza kikamilifu na kupata mahitaji ya msingi ya kielimu. Katika sura hii utajifunza dhana ya elimu jumuishi, malengo, misingi na historia ya elimu jumuishi Tanzania. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia misingi ya elimu jumuishi na kutoa fursa sawa kwa wanafunzi wote.*

### *Fikiri*

**Fursa za kujifunza kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu bila elimu jumuishi**

### Elimu jumuishi

Elimu jumuishi ni mfumo wa elimu unaotoa fursa kwa watu wote kama vile watoto, vijana, wazee na watu wazima kujiandikisha na kushiriki kikamilifu katika kujifunza darasani bila kujali tofauti zao za kimaumbile, kihali, kiakili, kijinsia au kikabila. Kwa ujumla, elimu jumuishi inalenga kutombagua mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu. Kwa umuhimu huu, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 uk.39 inasisitiza uboreshaji wa mazingira ya utoaji wa elimu jumuishi na kumwezesha kila Mtanzania kupata fursa za elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji yake. Hivyo, huu ni mchakato endelevu wa kuboresha mfumo wa elimu kwa kuondoa vikwazo katika upatikanaji wa elimu ili kuhakikisha wanafunzi wote wanasoma pamoja kwa kuzingatia mahitaji yao ya ujifunzaji. Aidha, ni mchakato wa kuongeza ushirikishwaji wa wanafunzi wote shuleni ikiwa ni pamoja na wenye mahitaji maalumu.

### Darasa Jumuishi

Darasa jumuishi ni darasa ambalo mwalimu na wanafunzi wanashirikiana katika shughuli mbalimbali na kujenga mazingira ambayo mwanafunzi anajisikia salama, anasaidiwa na kuhimizwa kutoa maoni yake na kuchangia katika ujifunzaji. Wanafunzi katika darasa jumuishi wana mahitaji tofauti na changamoto za ujifunzaji kama inavyoonesha kwenye kielelezo namba 1.1. Hivyo, ni muhimu kulifahamu darasa kwa idadi ya wanafunzi, tabia na mitindo yao ya ujifunzaji ili kutoa afua stahiki.

FOR ONLINE READING ONLY




Kielelezo namba 1.1: *Darasa jumuishi*

FOR ONLINE READING ONLY

## Sifa za elimu jumuishi

*Elimu jumuishi ni muhimu kwa sababu inaondoa vikwazo vinavyoweza kuathiri ushiriki wa wanafunzi katika kujifunza. Inawajengea ushirikiano na kuhakikisha kila mwanafunzi anapata elimu stahiki na yenye usawa. Zifuatazo ni sifa za elimu jumuishi:*

(a) *Usawa na Ujumuishaji: Huu ni mchakato unaohusisha wanafunzi wote kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kujifunza bila ubaguzi wowote;*

(b) *Kutambua mahitaji tofauti ya wanafunzi: Husaidia kutambua na kuheshimu tofauti za wanafunzi, ikiwa ni pamoja na tofauti za kiakili, kimwili na kijamii;*

(c) *Utoaji wa huduma: Huduma maalumu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ili kuhakikisha wanashiriki kikamilifu na kufanikiwa;*

(d) *Ushirikiano na mawasiliano kati ya walimu na wataalamu: Ushiriki wa wazazi, walimu na wataalamu kama vile wanasaikolojia katika kuhakikisha kila mwanafunzi anapata huduma zinazohitajika. Vilevile kupitia ushiriki na mawasiliano ya karibu, inasaidia katika kuboresha mchakato wa kujifunza na kuhakikisha kuwa mahitaji ya kila mwanafunzi yanatimizwa;*

(e) *Mazingira rafiki na wezeshi: Mazingira wezeshi ni jumla ya majengo, vifaa, na* rasilimali ambazo zinafikika kirahisi kwa wanafunzi wote; na

(*f*) *Mbinu nyumbufu za ufundishaji:* Matumizi ya mbinu fikivu na rafiki za ufundishaji zinazoendana na mahitaji ya ujifunzaji ya kila mwanafunzi.

### Umuhimu wa elimu jumuishi

Elimu jumuishi ina umuhimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ili kujenga maarifa, ujuzi na mwelekeo. Hii inasaidia wanafunzi wote kujifunza kuishi pamoja, kuelewana na kuthamini utofauti wao. Mshikamano huu utajenga jamii yenye uvumilivu na heshima kwa kila mtu, kukuza kujitegemea kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu na kujenga ujuzi wa kujitegemea katika mazingira jumuishi yanayoruhusu kushiriki kikamilifu katika shughuli zote. Vilevile elimu jumuishi ni muhimu kwa sababu inazingatia haki na usawa kwa kuhakikisha kila mwanafunzi anapata haki yake ya msingi ya elimu bila kujali tofauti zao za kimwili, kiakili au kijamii. Aidha, mfumo wa elimu jumuishi unalenga kutoa afua stahiki na kuweka mpango maalumu kwa mwanafunzi binafsi kama vile vifaa saidizi na zana za kujifunzia. Hii inasaidia kila mwanafunzi kufikia uwezo wake wa juu katika kujifunza.

### Kazi ya kufanya 1.1

Tembelea shule iliyo karibu, kisha fanya mahojiano na uongozi wa shule kuhusu utoaji wa elimu jumuishi ukihusisha faida na changamoto wanazozikabili. Andika nukuu za mazungumzo hayo kwa kutumia kinasa sauti kisha andika dondoo za mahojiano yenu na hifadhi kwenye mkoba wa kazi.

### Zoezi la 1.1

1. Umepangiwa shule inayotekeleza elimu jumuishi. Wakati wa kikao cha walimu na wazazi, umegundua kuwa wazazi wengi wanawaficha watoto wenye mahitaji maalumu nyumbani. Kama mwalimu mtaalamu eleza kwa nini elimu ni muhimu kwa watoto wenye mahitaji maalumu?
2. Elimu Jumuishi ina wajibu wa kukuza ujumuishi wa kijamii, kielimu na kiafya. Eleza sifa za elimu jumuishi katika jamii ya kitanzania kudhihirisha kauli hii?

### Malengo ya elimu jumuishi

Elimu jumuishi inalenga kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi, bila kujali uwezo wake au hali ya maisha, anapata fursa sawa ya kujifunza na kufanikiwa katika mazingira yanayomzunguka. Malengo ya elimu jumuishi yanakusudiwa katika maeneo yafuatayo:

(a) Kutoa elimu kwa watoto wote, wenye na wasio na mahitaji maalumu;

FOR ONLINE READING ONLY

(b) *Kuondoa vikwazo vya elimu nchini;*

(c) *Kujenga undugu, uzalendo na usawa;*

(d) *Kutoa fursa kwa wote kwa kuzingatia usawa wa jinsia; na*

(e) *Kujenga utamaduni wa kuheshimiana na kushirikiana.*

### Kazi ya kufanya 1.2

Serikali ya Tanzania imefanya jitihada za kufikia malengo ya maendeleo endelevu *kwa kuhakikisha wanafunzi wote wanapata elimu stahiki. Kama mdau wa elimu, tumia maktaba na vyanzo rasmi vya taarifa kueleza namna utekelezaji wa malengo hayo unavyoweza kusaidia kukuza stadi za karne ya 21 kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu.*

### Zoezi la 1.2

1. *Umetembelewa na wadau wa elimu jumuishi shuleni kwako wakihitaji taarifa za utekelezaji wa malengo ya elimu jumuishi kama yalivyoainishwa kwenye mkakati wa Taifa wa elimu jumuishi 2021/22-25/2026. Eleza namna unavyotekeleza malengo hayo katika ufundishaji na ujifunzaji kwenye darasa jumuishi.*

2. *Moja ya malengo ya elimu jumishi ni kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata elimu bila vikwazo. Eleza ni changamoto zipi zinakwamisha utoaji wa elimu* jumuishi kwa watoto wenye mahitaji maalumu nchini Tanzania na unafikiri nini *kifanyike ili kuzitatua.*

### Misingi ya elimu jumuishi

*Misingi ya elimu jumuishi ni muhimu katika kuweka kanuni na mikakati inayoshirikisha wanafunzi wote bila kujali tofauti zao za kiuwezo, kiuchumi na rangi. Msingi mkuu wa elimu jumuishi ni utoaji wa haki ya elimu kwa kila mwanafunzi mwenye na asiye na mahitaji maalumu. Hivyo basi, msingi huu unatambua ni vema kuwa na vigezo vinavyozingatia ujumuishi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Misingi ya elimu jumuishi husisitiza yafuatayo:*

(a) *Kila mwanafunzi ana uwezo wa kujifunza;*

(b) *Kila mwanafunzi ana haki ya kushiriki katika zoezi la ujifunzaji;*

(c) *Kila mwanafunzi ana namna yake ya kujifunza na kujieleza;*

FOR ONLINE READING ONLY

(d) Matumizi ya zana na mbinu nyumbufu za ufundishaji na ujifunzaji;

(e) Kuwepo kwa mazingira rafiki na fikivu ya ujifunzaji kwa mwanafunzi; na

(f) Kuwepo kwa huduma stahiki kwa makundi ya watoto wenye mahitaji maalumu.

### Kazi ya kufanya 1.3

Kama mtaalamu wa elimu jumuishi, eleza tofauti ya misingi na malengo ya elimu jumuishi na andika insha isiyopungua maneno mia tano. Tumia maktaba na vyanzo rasmi vya taarifa mtandaoni kupata maarifa. Kisha, hifadhi insha yako kwenye mkoba wa kazi.

### Zoezi la 1.3

1. Kwa kutumia mifano eleza misingi ya elimu jumuishi inavyotekelezwa katika chuo chako.
2. Katika kufikia lengo la ufundishaji na ujifunzaji wa elimu jumuishi ni muhimu kuzingatia misingi yake. Kwa kutumia mifano eleza namna utekelezaji wa misingi ya elimu jumuishi ulivyoleta mabadilikio ya ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu chuoni kwako.

### Historia ya elimu jumuishi Tanzania

Elimu jumuishi ilianza kutolewa nyumbani ikirithishwa kutoka kizazi kimoja mpaka kingine. Elimu rasmi shuleni ilianza kutolewa kuanzia karne ya 14. Mnamo miaka ya 1700 wanaharakati mbalimbali walianza kutetea elimu kwa watu wenye ulemavu. Kufikia miaka ya 1950, watu wenye ulemavu nchini Tanzania walikuwa wakipata elimu kupitia mfumo rasmi kwenye shule maalumu. Elimu kwa watu wenye ulemavu nchini Tanzania ilianza kutolewa kwa watoto wenye ulemavu wa uoni ikifuatiwa na ulemavu wa uziwi. Baadaye shule za watoto wenye ulemavu wa viungo zilifunguliwa na kufuatiwa na shule za watoto wenye ulemavu wa akili. Kwa mara ya kwanza shule hizi zilianzishwa na wamisionari, wasamaria na wanaharakati wa kigeni. Baada ya uhuru Serikali ya Tanzania ilifanya ugatuzi wa shule hizo na kuanzisha shule nyingine za watoto wenye ulemavu. Kutokana na elimu maalumu kuwakosesha watu wenye ulemavu haki ya kuchangamana na wenzao, wanaharakati wa haki za binadamu, wataalamu na wadau mbalimbali wa elimu waliamua kusisitiza suala la elimu jumuishi.

FOR ONLINE READING ONLY

## Kazimradi 1.1

Chunguza hali ya utekelezaji wa elimu jumuishi katika shule ya msingi iliyopo karibu. Tumia maswali yafuatayo kupata majibu yatakayokusaidia kuandikia ripoti. Aidha, taarifa yako ihusishe mbinu uliyotumia kukusanya na kuchambua data. Weka taarifa yako kwenye mkoba wa kazi.

1. Taja mambo yaliyobainishwa na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 kuhusu elimu jumuishi?
2. Ni changamoto gani kubwa zinakwamisha utoaji wa elimu jumuishi nchini Tanzania?
3. Mafanikio gani yamepatikana katika utekelezaji wa elimu jumuishi?
4. Ni mkakati gani unaweza kutumika kuboresha utoaji wa elimu jumuishi nchini Tanzania?

### Chimbuko la elimu jumuishi nchini Tanzania

Elimu jumuishi imeanza kutekelezwa nchini Tanzania kupitia Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 iliyoelekeza upatikanaji wa elimu kwa kila mtoto. Utekelezaji wa sheria hii kwa watoto wenye mahitaji maalumu umerasimishwa mwaka 1998 kupitia mradi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Utamaduni kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Elimu, (UNESCO). Mradi huo ulitambulika kama "Special Needs in the Classroom", na ulifanyika katika shule za Mkoa wa Dar es Salaam. Mradi huu pia ulitoa elimu kwa walimu na wazazi kuhusu umuhimu na namna ya kutekeleza elimu jumuishi. Moja ya matokeo ya mradi huu ni kuandaliwa kwa Mkakati wa elimu jumuishi wa Mwaka 2009-2017. Hata hivyo, Serikali imeendelea kuboresha na kuandaa mikakati ya Taifa ya elimu jumuishi ikiwa ni pamoja na Mkakati wa Elimu Jumuishi wa Mwaka 2022-2026. Ikumbukwe kwamba, Tanzania imeridhia mikataba ya kimataifa na kutunga sera na sheria mbalimbali za kitaifa zinazoelekeza utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi shuleni. Mikataba, sera na sheria hizi zinafafanuliwa kama ifuatavyo:

### Mikataba ya kimataifa

(a) *Mkataba wa haki za watoto 1989 (UN Convention on the Rights of the Child):* Azimio hili lililenga kutetea haki za watoto wote wapate elimu bila ubaguzi wa aina yeyote ndani ya kifungu cha 28 na 29. Katika kifungu cha 28 inasisitizwa elimu msingi kuwa ni ya lazima na bure kwa wote na elimu ya sekondari ilifanywa kuwa bure kwa baadhi ya hatua. Aidha mkakati huu

FOR ONLINE READING ONLY

ulihakikisha unapunguza idadi ya watoto wanaoacha shule. Kifungu cha 29 kinasisitiza kukuza uwezo wa mtoto, na kumfanya kuwa raia anayewajibika katika jamii yenye usawa, amani na uvumilivu. Pia kuhakikisha wazazi na watoto wanaheshimiwa kulingana na tamaduni zao;

(b) *Jomtien Declaration 1990:* Mkutano wa Jomtien uliweka msisitizo mkubwa juu ya upatikanaji wa elimu kwa watu wote duniani, hasa kwa wale walio katika mazingira magumu na waliotengwa. Hii ilitokana na mkutano wa elimu kwa wote uliofanyika Jomtien, Thailand. Azimio hili linatambua kuwa kila mtu, bila kujali hali yake ya kijamii, kiuchumi, au kisiasa ana haki ya kupata elimu. Elimu inachukuliwa ni haki ya msingi ya binadamu;

(c) *Salamanca Declaration 1994:* Azimio la Salamanca la mwaka 1994 lilizungumzia haki ya elimu kwa wote. Pia, lilisisitiza kila mtoto kuwa na haki ya kupata elimu bila ubaguzi wowote. Elimu jumuishi ihusishe watoto wenye mahitaji maalumu. Ujumuishi huu uhusishe kufanya utambuzi wa awali, upimaji na utoaji wa afua stahiki;

(d) *Dakar Framework for Action 2000:* Mkutano wa Dakar uliweka msisitizo wa elimu kwa wote. Ambapo ulisisitiza haki ya kila mtu kupata elimu bora bila kujali hali yake ya kijamii, kiuchumi, kimaumbile au kiumri. Hii inajumuisha kuondoa vikwazo vyote vinavyozuia watoto, vijana na watu wazima, hasa wale wanaotoka familia maskini na wenye ulemavu kupata elimu. Pia, mkutano ulisisitiza kuwa na mazingira ya kujifunzia ambayo ni salama na yenye rasilimali zinazofaa. Aidha, mkutano huo ulisisitiza kuimarisha mipango ya kitaifa ili kufanikisha malengo ya elimu. Kwa ujumla, mkutano wa Dakar ulitaka kujenga mfumo wa elimu unaojumuisha na unaowezesha kila mtu kufikia fursa za kujifunza.

(e) *Mkataba wa umoja wa mataifa kuhusu haki za watu wenye ulemavu 2006 (UN Convention on the Rights of Persons with Disabilities):* Mkataba huu ulilenga kulinda, kukuza, na kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata haki zao kikamilifu, ikiwa ni pamoja na haki ya elimu. Mwaka 2006 Mkataba ulipitishwa na kuanza kutumika mwaka 2008. Ulijikita katika kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanahusishwa kikamilifu katika jamii na maendeleo kwa njia jumuishi; na

(f) *Malengo ya maendeleo endelevu ya Mwaka 2030:* Malengo ya maendeleo endelevu yalizungumzia elimu jumuishi na usawa kwa wote. Pia yalisisitiza, kufikia mwaka 2030 wanafunzi wote wasichana na wavulana kukamilisha elimu yao ya msingi na sekondari ambayo itakuwa ni bure. Elimu hii itakuwa na usawa, yenye ubora na inayoleta matokeo chanya ya ujifunzaji. Hata hivyo,

FOR ONLINE READING ONLY

malengo ya maendeleo ya Mwaka 2030 yanatoa dira ya usawa wa elimu kwa makundi yote bila ubaguzi na hii imekuwa chachu kubwa kwa Tanzania kutekeleza maagizo ya mikataba hiyo.

### Sera na sheria za kitaifa

(a) *Sera ya Taifa ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2004:* Sera hii iliandaliwa nchini Tanzania ikilenga kuimarisha haki na ustawi wa watu wenye ulemavu, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba wanapata huduma muhimu kama elimu, afya, na ajira bila kubaguliwa. Kuhusu elimu, sera hii inatoa mwongozo wa kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata elimu bora na ya usawa, ili waweze kujitegemea na kushiriki kikamilifu katika jamii;

(b) *Mkakati wa elimu jumuishi Tanzania 2009-2017:* Huu ni mkakati wa kwanza wa elimu jumuishi kutengenezwa nchini Tanzania. Mkakati huu uliweka programu zinazolenga kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wakiwemo wale wenye mahitaji maalumu wanapata elimu bora na ya usawa. Mkakati huu ulifuatiwa na mkakati wa elimu jumuishi wa mwaka (2018-2021 na 2021/2022 – 2025/2026);

(c) *Sheria ya watu wenye ulemavu 2010 (The persons with disabilities Act):* Sheria hii ilipitishwa nchini Tanzania ili kulinda haki za watu wenye ulemavu na kutoa mwongozo wa utekelezaji wa hatua mbalimbali zinazohusiana na ustawi wao. Katika kifungu namba 8, sheria inazungumzia umuhimu wa elimu kwa watu wenye ulemavu na imeweka misingi ya kuhakikisha kuwa watu hawa wanapata haki ya elimu kwa usawa na kwa kuzingatia mahitaji yao maalumu;

(d) *Sera ya elimu na mafunzo Tanzania 2014:* Sera hii inaelezea haki ya elimu kwa wote. Sera imeweka msingi wa kuhakikisha elimu inapatikana kwa watoto wote bila kujali hali zao za kimwili, kiakili na kijamii. Sera ya elimu inasisitiza umuhimu wa elimu jumuishi kama sehemu ya haki za binadamu na maendeleo ya kijamii na kuweka msingi wa elimu bila malipo kwa wanafunzi wote; na

(e) *Mpango wa maendeleo ya sekta ya elimu (2016-2017)-(2020-2021):* Mpango huu ulilenga kuongeza ushirikishwaji wa watoto wenye mahitaji maalumu katika mfumo wa kawaida wa elimu kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kielimu zinazokidhi mahitaji yao. Vilevile iliweka mpango wa elimu kwa watu wenye ulemavu ambao ulikuwa sehemu ya juhudi za serikali za kuboresha upatikanaji wa elimu kwa watoto wenye ulemavu.

FOR ONLINE READING ONLY

## Kazi ya kufanya 1.4

Kwa kutumia makala yanayotoka katika tovuti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, maktaba na vyanzo rasmi mtandaoni, chambua utekelezaji wa elimu jumuishi nchini Tanzania. Andika dondoo na hifadhi katika mkoba wako wa kazi.

## Zoezi la marudio

1. Elimu jumuishi inazingatia vigezo mbalimbali ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wakiwemo wenye mahitaji maalumu wanapata elimu stahiki. Eleza mambo ya kuzingatia ili kukuza ujumuishi katika jamii ya kitanzania.
2. Elimu jumuishi inahamasisha utoaji elimu kwa wote. Kutokana na msisistizo huo, eleza umuhimu wa elimu jumuishi.
3. Serikali ya Tanzania imefanya jitihada za kufikia malengo ya maendeleo endelevu kwa kuhakikisha watoto wote wanapata elimu stahiki. Eleza mikakati iliyofikiwa na Serikali ili kufanikisha malengo hayo.
4. Umealikwa kushiriki mdahalo wa elimu, mada inayowasilishwa ni elimu ya kuondoa unyanyapaa. Eleza ni mambo gani utakayozungumza ambayo yataondoa unyanyapaa katika kutekeleza elimu jumuishi.
5. Kwa kuzingatia matamko muhimu yaliyoridhiwa na mkutano wa Salamanca wa mwaka 1994, eleza kwa mifano utekelezaji wa elimu jumuishi nchini Tanzania.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Pili

# Utambuzi wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu

## Utangulizi

*Utambuzi wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ni muhimu katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji darasani. Hatua hizi hufanyika awali pale mwanafunzi anapoanza mafunzo yake ili kumsaidia mwalimu kutoa afua stahiki itakayomwezesha mwanafunzi kujifunza kwa ufanisi. Katika sura hii utajifunza dhana ya mahitaji maalumu, utambuzi wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu, viashiria vya mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu na mbinu na zana za ubainishaji wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia mbinu na zana mbalimbali za ubainishaji wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji.*

## *Fikiri*

**Mambo ya kuzingatia katika darasa jumuishi**

FOR ONLINE READING ONLY

## Dhana ya mahitaji maalumu

Mahitaji maalumu ni huduma za ziada kwa mtu ili kumwezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za kila siku. Mahitaji haya yanaweza kutokana na hali za ulemavu, afya, kijamii, kiakili au kihisia ambazo zinaweza kuathiri uwezo wao wa kufanya kazi. Hivyo, ili mtu aweze kutenda shughuli au kazi, anahitaji kupewa huduma stahiki itakayomwezesha kutekeleza jukumu hilo. Mfano wa huduma hizi zinaweza kuhusisha vifaa saidizi kama vile magongo, fimbo nyeupe, vifaa vya kukuza usikivu, ushauri na unasihi pamoja na matibabu.

### Aina za mahitaji maalumu

Mahitaji maalumu yanaweza kuainishwa katika maeneo tofauti kulingana na ulemavu au changamoto alizonazo mwanafunzi. Zifuatazo ni changamoto zinazosababisha aina za mahitaji maalumu:

(a) *Changamoto za ujifunzaji:* Hivi ni vikwazo vinavyoweza kuathiri mchakato wa elimu kwa mwanafunzi, ambapo wanafunzi hawa wanaweza kukabiliwa na

matatizo mbalimbali. Kwa mfano, wanaweza kushindwa kusoma kwa ufanisi wakichanganya herufi kama "u" na "n," au "b" na "d," hali hii inajulikana kama disleksia. Aidha, baadhi yao wanapata changamoto katika kuandika, inayojulikana kama disgrafia, na wengine wanashindwa kujifunza kuhesabu, jambo linalojulikana kama diskalkulia. Wanafunzi wengine wanaweza kukumbwa na ugumu katika kuelewa lugha na kuzungumza, changamoto hii inajulikana kama afasia. Pia, kuna wanafunzi wanaokabiliwa na ugumu wa kutekeleza vitendo vya kawaida kwa usahihi, inayojulikana kama apraksia, na wengine wanapata changamoto za matamshi, inayoitwa disathria. Mbali na hayo, baadhi yao wanakabiliwa na matatizo ya kutunza kumbukumbu, kuona aibu na kushindwa kujiamini. Hata hivyo, wanafunzi wenye vipaji maalumu wanaweza kuonesha uwezo wa juu wa kufikiri, kubuni, au kutenda katika nyanja kama sanaa, muziki, michezo, sayansi, hisabati na lugha. Wanaweza kujifunza kwa haraka, hivyo wanahitaji mbinu maalumu za elimu ili kukuza uwezo wao kwa kiwango cha juu zaidi. Hali hizi zinahitaji umakini kutoka kwa walimu na jamii kwa ujumla ili kuwasaidia wanafunzi hawa kufikia uwezo wao kamili katika mazingira ya kujifunza;

(b) *Changamoto za mawasiliano:* Hujitokeza wakati mwanafunzi anajaribu kuwasiliana lakini hukutana na vikwazo ambavyo vinazuia kuelewa au kupokea ujumbe kwa usahihi. Hii husababishwa na uziwi, ulemavu wa kuona na ulemavu wa matamshi;

(c) *Changamoto za kihisia, kitabia na kijamii:* Huhusisha hisia za mtu binafsi na jinsi anavyohusiana na wengine na kusababisha kutoshirikikiana au kuchangamana katika jamii. Vilevile, watu wanaokabiliwa na changamoto hii huwa na changamoto ya afya ya akili kwa sababu ya kuwa na wasiwasi au uwoga uliopitiliza, huzuni, hasira, unyonge, kutengwa na jamii, unyanyasaji na ubaguzi. Hali hii hutokana na historia ya malezi, makuzi na mazingira ya mwanafunzi husika;

(d) *Changamoto za kimaumbile:* Ulemavu huu unahusisha watu wenye ulemavu wa viungo, kusinyaa kwa misuli, mgongo wazi na wanahitaji msaada wa kimaumbile kama vile kutumia magongo, kitimwendo, au vifaa vingine saidizi;


(e) *Changamoto za kiakili:* Zinahusisha hitilafu mbalimbali katika ubongo na mfumo wa neva ambazo zinaweza kuonekana katika matumizi ya lugha, kukumbuka, kujifunza, kuelewa tatizo na kutafuta suluhisho; na

(f) *Changamoto za kiafya:* Hujumuisha watu wenye magonjwa sugu kama vile kisukari, ugonjwa wa moyo na saratani na wanahitaji uangalizi maalumu.

FOR ONLINE READING ONLY

## Makundi ya watu wenye mahitaji maalumu

*Utoaji wa elimu jumuishi nchini unatambua kuwepo kwa makundi mbalimbali ya watu wenye mahitaji maalumu ambao wanahitaji umakini katika kupewa elimu. Makundi haya yanatokana na changamoto ambazo watu wenye mahitaji maalumu wamekuwa wakikutana nazo katika jamii. Hivyo, ni muhimu kufahamu mahitaji ya mwanafunzi ya ujifunzaji katika kila kundi ili kutoa afua stahiki. Kielelezo namba 2.1 kinaonesha makundi ya watu wenye mahitaji maalumu.*




Kielelezo namba 2.1*: Makundi ya watu wenye mahitaji maalumu*

FOR ONLINE READING ONLY

## Kazi ya kufanya 2.1

Tembelea shule iliyoko jirani kisha jadiliana na walimu wa shule hiyo kuhusu makundi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu walioko katika mazingira yao. Kisha andika nukuu kwa kuzingatia yafuatayo;

1. Aina ya ulemavu
2. Jinsia
3. Umri wake
4. Darasa alilopo
5. Chagamoto ambazo mwanafunzi wanakutana nazo katika ujifunzaji.

Kisha hifadhi kazi yako kwenye mkoba wa kazi.

## Zoezi la 2.1

1. Mwanafunzi mwenye ulemavu anachangamoto katika kuzungumza, kusoma, kuandika, kufikiri na kuhesabu. Kama mtaalamu, orodhesha viashiria vitakavyokusaidia kumbaini mwanafunzi huyo darasani.
2. Mwalimu wa elimu jumuishi anao uwezo wa kuainisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Eleza changamoto zinazotokana na aina ya mahitaji maalumu kijamii, kihisia na kitabia.
3. Elimu jumuishi haihusiani na wanafunzi wenye ulemavu pekee, bali hujihusisha na wenye changamoto nyingine za kimaisha. Eleza makundi mengine zaidi ya yale yaliyotajwa katika sura hii ambayo yanapaswa kujumuishwa katika elimu jumuishi.

## Utambuzi wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji

Huu ni mchakato wa kutambua na kuelewa mahitaji maalumu ya kitaaluma au kisaikolojia ya mwanafunzi ambaye anakutana na changamoto katika mchakato wa ujifunzaji. Mahitaji haya maalumu yanaweza kuwa ya kitaaluma, kihisia, kimaumbile, kiakili au kijamii. Pia utambuzi unahusisha kubaini changamoto za ujifunzaji au za kimaendeleo katika hatua za awali kama vile changamoto za lugha, ulemavu wa kimaumbile na kitabia. Aidha, mchakato huu unalenga kuwezesha utekelezaji wa mikakati ya utoaji wa afua stahiki kabla ya changamoto hizo kuwa kubwa. Zifuatazo ni hatua za utambuzi:

(a) Kutambua dalili za awali: Walimu, wazazi, na wataalamu wengine kubaini

FOR ONLINE READING ONLY

dalili za awali za changamoto za ujifunzaji kupitia utendaji wa mwanafunzi;

(b) *Kufanya uchunguzi na tathmini:* Mchakato huu unafanyika baada ya kutambua dalili na kufanya uchunguzi wa kitaalamu ili kuthibitisha kama mwanafunzi ana mahitaji maalumu. Hii inaweza kujumuisha tathmini za kielimu, kisaikolojia, au za kitabibu;

(c) *Kuandaa mpango wa huduma:* Mpango huu hufanyika mara baada ya kugundua mahitaji ya mwanafunzi. Timu ya elimu ikiwa ni pamoja na walimu, wazazi, na wataalamu huandaa mpango binafsi wa ujifunzaji au mpango wa huduma ili kuhakikisha mwanafunzi anapata mahitaji stahiki; na

(d) *Kuandaa mazingira jumuishi:* Hatua ambayo inachukuliwa katika kuandaa mazingira rafiki na wezeshi ili kuhakikisha ushirikishwaji wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu katika ujifunzaji.

### Kazi ya kufanya 2.2

Tembelea maktaba ya chuo pamoja na vyanzo rasmi vya taarifa, chunguza jinsi hatua za utambuzi wa mahitaji maalumu zinavyofanyika. Andika dondoo na hifadhi katika mkoba wa kazi.

### Zoezi 2.2

1. Eleza vitu vya msingi vya kuzingatia wakati wa utambuzi wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu.
2. Changanua vipengele muhimu vilivyomo kwenye fomu ya ubainishaji wa utambuzi wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu.

## Viashiria vya mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu

Viashiria vya mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ni dalili zinazomwezesha mwalimu kumtambua mwanafunzi huyo. Mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu anaweza kuwa na changamoto ambazo zinahitaji uelewa wa kina ili kumsaidia kufanikiwa kimasomo na kijamii. Hivyo, kufahamu viashiria vya mwanfunzi huyo ni muhimu katika kubaini mahitaji yake na kutoa huduma stahiki. Vifuatavyo ni viashiria vya mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu:

(a) *Kiashiria katika kujifunza:* Mwanafunzi anaweza kuonesha ugumu wa kuelewa au kukumbuka maelekezo, kuchelewa kujifunza mambo mapya, au kutojua kabisa baadhi ya dhana. Aidha, mwanafunzi mwenye kipaji na kipawa cha kipekee anaweza kuelewa kwa haraka dhana mpya na msamiati wakati

FOR ONLINE READING ONLY

wa kujifunza, kukosa utulivu kutokana na kazi zisizotosheleza na anapenda kudakia na kuingilia mambo kabla ya wakati wake;

(b) *Tofauti za kitabia, kihisia na kijamii:* Mwanafunzi anaweza kuonesha hisia kali kama vile hasira au huzuni bila sababu inayoonekana. Pia, anaweza kujitenga na jamii, kujiamini kupita kiasi na kuishi katika mazingira hatarishi. Hii hutokana na historia ya malezi, makuzi na mazingira ya mwanafunzi husika, mfano watoto wa mtaani;

(c) *Ulemavu wa milango ya fahamu:* Mwanafunzi anaweza kuwa na changamoto katika kuzungumza, kusikiliza, kuona, kuelewa lugha, au kuchangamana na wenzake. Hali hii inaweza kuathiri mawasiliano kati ya mwanafunzi na walimu, mwanafunzi na wanafunzi wenzake au mwanafunzi na jamii inayomzunguka; na

(d) *Tofauti ya kimaumbile:* Mwanafunzi anaweza kuwa na ulemavu wa viungo kwa mfano, ulemavu wa miguu, mikono, au ulemavu mwingine wa kimaumbile. Hali hii huathiri uwezo wa kudhibiti mwendo wa misuli ambayo huzuia ujongeaji, na kutokufanya kazi ipasavyo unaomfanya asiweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za kawaida za darasani.

## Kazi ya kufanya 2.3

Tembelea shule iliyo karibu na chuo kisha chunguza fomu ya maendeleo ya mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kuona ni hatua zipi zimechukuliwa baada ya ubainishaji na afua stahiki iliyotolewa. Andika taarifa kisha hifadhi kwenye mkoba wa kazi.

## Zoezi la 2.3

1. Kwa kutumia mifano eleza viashiria vinavyoweza kusaidia kuwatambua wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika darasa jumuishi.
2. Kwa kutumia mifano eleza tofauti kati ya wanafunzi wenye vipaji na wenye vipawa.
3. Mwanafunzi mwenye changamoto ya mawasiliano hushindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za darasani. Eleza mbinu unazoweza kuzitumia ili kuboresha ushiriki wake katika shughuli za vikundi.
4. Wakati wa ufundishaji na ujifunzaji darasani umegundua mwanafunzi mmoja anapenda kukutazama usoni muda wote. Eleza kwa kutumia utaalamu ni changamoto ipi aliyonayo mwanafunzi huyo.

FOR ONLINE READING ONLY

5. Bainisha viashiria vya ulemavu wa akili na usonji vinavyomsaidia mwalimu kutoa elimu ya ufahamu kwa wazazi na walezi wenye wanafunzi hao.

## Mbinu za ubainishaji wa mapema kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji

Ubainishaji wa mapema ni muhimu katika kutambua mahitaji ya mwanafunzi ya ujifunzaji, uwezo na vipawa vyake. Ubainishaji unaweza kufanywa kwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira halisi na huhusisha matumizi ya mbinu mbalimbali kulingana na aina ya ulemavu au changamoto ya mwanafunzi. Zifuatazo ni mbinu za ubainishaji wa mapema:

(a) *Uchunguzi wa awali:* Unafanywa kwa wanafunzi wote ili kubaini viashiria vya awali vya changamoto ya ujifunzaji. Mfano, uchunguzi wa afya ya mwanafunzi unafanyika kupima kama ana uoni hafifu, usikivu duni, tabia na magonjwa mengine ukihusisha upimaji wa stadi za msingi za kusoma, kuandika, na kuhesabu. Uchunguzi huu ni wa haraka na rahisi kutekeleza na mara nyingi hutumiwa kama hatua ya kwanza;

(b) *Tathmini ya kibinafsi:* Hufanyika kwa mwanafunzi aliyethibitika kuwa na changamoto baada ya uchunguzi wa awali. Mwanafunzi atapimwa ili kubaini uwezo wake wa kujifunza.Tathmini hii inalenga kuelewa changamoto anayokutana nayo, na kutathmini ujifunzaji wake katika masomo kama vile lugha, hisabati, sayansi, na stadi za maisha; na

(c) *Historia ya familia na changamoto ya afya:* Hali ya kiafya ya mwanafunzi inaweza kutoa mwanga kuhusu chanzo cha changamoto ya ujifunzaji. Hivyo, changamoto hizi zinaweza kubainishwa kwa kukusanya taarifa ya kiafya, kimasomo na kijamii kutoka kwenye familia ya mwanafunzi. Hii inaweza kujumuisha mahojiano na wazazi, walimu na wadau wengine ili kupata mtazamo kamili wa changamoto za mwanafunzi.

### Kazimradi 2.1

Tembelea shule ya msingi iliyo karibu na chuo chako inayotekeleza mfumo wa elimu jumuishi. Tumia maswali yafuatayo kupata majibu yatakayokusaidia kuandika taarifa yako inayohusu mbinu ulizozitumia katika ubainishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, kisha hifadhi kwenye mkoba wa kazi.

1. Kwa nini tunawapima wanafunzi?
2. Kwa nini ni muhimu kutambua mahitaji ya ujifunzaji?
3. Nani anayehusika na kufanya tathmini ya mahitaji ya ujifunzaji?

FOR ONLINE READING ONLY

4. Ni wakati gani inapendekezwa kufanya tathmini ya mahitaji ya ujifunzaji?
5. Tathmini ya mahitaji ya ujifunzaji inafanywa vipi?
6. Ni changamoto gani zinajitokeza katika kupima wanafunzi ili kubaini mahitaji yao?

## Zana za ubainaishaji wa mapema kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji

Zana za ubainishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ni vifaa vinavyotumika kutambua aina ya changamoto aliyonayo mwanafunzi ili kuweza kumsaidia katika ujifunzaji. Aidha, zana hizi zinaweza kutumika kumbaini mwanafunzi mwenye changamoto zaidi ya moja. Zifuatazo ni zana za ubainishaji wa mapema kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji pamoja na matumizi yake:

### Zana zinazotumika katika ubainishaji wa mwanafunzi mwenye uziwi

(a) *Manyanga:* Hutumika kutoa sauti kwa kutikiswa nyuma ya mtoto mwenye uziwi ili kungundua uwezo wake wa kusikia sauti. Manyanga hutumika kupima kiwango cha uziwi kwa watu wa rika zote. Hii husaidia wataalamu wa afya ya masikio kubaini aina na kiwango cha uziwi.

#### Namna ya kutumia manyanga

Kutumia seti ya manyanga yenye mzunguko tofauti wa sauti za juu na chini ambazo zinaweza kufanya upimaji katika mazingira tulivu ili kuhakikisha mwanafunzi anaweza kusikia sauti kwa usahihi bila vikwazo vya kelele za nje. Vilevile, atapata maelekezo ya awali kuhusu zoezi ambalo sio hatarishi kwake. Manyanga yatapigwa katika kichwa cha mwanafunzi, sehemu ya mifupa karibu na sikio, kwenye paji la uso au nyuma ya sikio. Mwanafunzi asiposikia sauti inayotokana na manyanga au kutoitambua sauti hiyo, ni dalili ya changamoto ya usikivu.

(b) *Zomali, vuvuzela na filimbi:* Zana ya zomali, ni kifaa kinachopulizwa na kinachozalisha sauti kali. Zana hii hupima mawimbi ya juu. Hivyo, kama mwanafunzi atashindwa kuitika itaonesha anachangamoto ya kusikia iliyosababishwa na sikio la ndani. Vilevile, vuvuzela hutoa sauti kubwa inayoweza kuzalisha mtetemo wenye nguvu. Filimbi ni kifaa chenye sauti nyembamba, ambayo hutumika kupima mawimbi ya sauti za juu. Mwanafunzi akishindwa kupokea mawimbi ya sauti hizo, atabainishwa kuwa na changamoto ya usikivu.

FOR ONLINE READING ONLY

**Namna ya kutumia zomali, vuvuzela na filimbi**

Zana hizi, zinatumika kutoa sauti na kusikika kwa urahisi. Vilevile zinatumika kwenye mazingira ambayo hayana kelele ili mwanafunzi asisumbuliwe na sauti za nje. Mwanafunzi atapata maelekezo ya awali kuhusu zoezi ambalo sio hatarishi kwake. Aidha, wakati wa mchakato huu, mwanafunzi anasimama umbali ambao ataweza kusikia, mfano mita moja kutoka kwa mwalimu ili sauti ya kila zana hiyo isikike bila shida. Mwitikio wa mwanafunzi unaweza kuhusisha kugeuka, kuonesha alama ya kusikia, au kutoa maoni kama amesikia.

(c) *Ngoma:* Hutumika kubaini mwanafunzi mwenye uziwi na ni njia rahisi ya kiasili katika mazingira ya shule. Sauti ya ngoma ni nzito na yenye mitetemo ambayo inaweza kusaidia kubaini kama mwanafunzi ana changamoto ya usikivu.

### Kazi ya kufanya 2.4

Wewe kama mtaalamu wa elimu jumuishi umealikwa kuwawezesha walimu wa shule ya msingi namna watakavyo wabaini wanafunzi wenye uziwi. Kwa kutumia mifano eleza mambo muhimu yakuzingatia ili waweze kuwabaini wanafunzi hao. Hifadhi kazi hii kwenye mkoba wa kazi.

### Zoezi la 2.4

Hatua za ubainishaji wa mwanafunzi mwenye changamoto ya usikivu zinaweza kufanywa na mwalimu mwenyewe. Eleza jinsi utakavyotumia zana ya ngoma kumbaini mwanafunzi kiziwi.

### Zana zinazotumika katika ubainishaji wa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni

(a) *LEA chati:* Alama zinaandikwa kwenye karatasi ngumu na hutumika kupima mwanafunzi mwenye changamoto ya uoni.

**Namna ya kutumia LEA chati**

Chati hii inatumika pale mwanafunzi anaposhauriwa kusimama umbali wa mita 3 hadi 6 kwenye usawa wa macho yake na kueleza alama anazoziona kwenye chati. Anaweza kutumia macho yote mawili kusoma chati wakati akioneshwa alama kubwa juu na kushuka chini polepole hadi pale anaposhindwa kuona

FOR ONLINE READING ONLY

vizuri. Hatua inayofuata katika zoezi hili, jicho moja litafunikwa kwa kipande cha karatasi au kifaa kingine na kusoma chati kwa kutumia jicho lililobaki wazi. Vilevile, zoezi hili litarudiwa kwa jicho la pili. Mwanafunzi akishindwa kusoma alama kwa usahihi, atabainishwa kuwa na changamoto ya uoni.

(b) *Uzi wa brock:* Uzi wenye urefu wa takriban futi 10 wenye shanga kubwa za rangi tofauti kama vile nyekundu, kijani, njano, nyeusi na bluu zilizowekwa kwenye uzi huo. Uzi unaotumika uwe wa rangi tofauti na zile zilizopo kwenye shanga.

### Namna ya kutumia uzi wa Brock

Mwanafunzi anashikilia ncha ya mwisho ya uzi karibu na pua yake, na mwisho mwingine unashikiliwa au kufungwa kwenye kitu imara mbele ya mwanafunzi. Uzi unakuwa katika mstari ulionyooka kati ya macho ya mwanafunzi na kitu kilichofungwa.

Mchakato huu utahusisha kuangalia shanga iliyo mbele katika uzi karibu na pua kwa kutumia macho yote mawili. Kama macho yote yanafanya kazi kwa pamoja, mwanafunzi ataona uzi umetengeneza umbo la 'V' au umbo la 'X' ikiwa anaangalia shanga ya kati. Hatua hii inarudiwa kwa shanga inayofuata ya kati. Ikiwa mwanafunzi anaona uzi kama msitari mmoja baada ya kuonekana kugawanyika kwenye shanga, hii inaweza kuashiria kuwa macho yake yana changamoto ya uoni. Matokeo haya yanaweza kusaidia kuamua kama mwanafunzi anahitaji uchunguzi zaidi kutoka kwa mtaalamu wa macho.

(c) *Mpira na ndoo:* Hizi ni zana ambazo zinatumika kubaini changamoto za uoni kwa mwanafunzi katika uwezo wa kuona mbali kwa usahihi.

### Namna ya kutumia mpira na ndoo

Matumizi yanajumuisha mpira mdogo na ndoo, kwa kuweka ndoo umbali wa takribani mita 3 hadi 5 kutoka kwa mwanafunzi. Mwanafunzi anarusha mpira kuelekea kwenye ndoo akilenga mpira kuingia ndani ya ndoo hiyo bila kusaidiwa. Aidha, hatua inayofuata mwanafunzi anatumia jicho moja kwa kutumia kiganja chake au kipande cha kitambaa kurusha mpira kwenye ndoo. Matokeo ya kila jaribio yanakiliwe ili kufanya tathmini ya zoezi lote. Mwanafunzi akishindwa kulenga mpira ndani ya ndoo kwa kurudia, hii inaweza kuashiria changamoto ya kuona mbali.

FOR ONLINE READING ONLY

## Kazi ya kufanya 2.5

Wakati wa ufundishaji darasani, umegundua mwanafunzi mmoja anachangamoto ya uoni. Eleza zana utakayotumia kubaini changamoto ya uoni na afua stahiki utakayoitoa katika changamoto hiyo. Andaa taarifa na hifadhi katika mkoba wa kazi.

## Zoezi la 2.5

1. Eleze maana ya zana ya LEA chati na namna utakavyotumia kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.
2. Mwanafunzi mwenye ualbino anachangamoto ya kuona mbali. Ukiwa kama mtaalamu wa elimu maalumu eleza zana zitakazotumika kumbainisha mwanafunzi huyo.

### Zana zinazotumika katika ubainishaji wa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwenye usonji

(a) *Mwanasesere:* Zana hii hutumika kumwezesha mwanafunzi kubaini sehemu za mwili. Iwapo mwanafunzi atashindwa kuonesha eneo sahihi atabainishwa kuwa na ulemavu wa akili.

#### Namna ya kutumia mwanasesere

Zoezi hili litahusisha mwanafunzi kuchezea mwanasesere na kuigiza vitendo kama vile kumpatia mwanasesere chakula, kumvika nguo, au kumpeleka kulala. Tathmini itafanyika kuona mwanafunzi anavyoweza kufuata maagizo rahisi, kuelekezwa na jinsi anavyoweza kuonesha hisia au matendo ya kijamii akicheza na mwanasesere huyo. Mwanafunzi akishindwa kufanya vitendo rahisi vya uigizaji wakati anacheza na mwanasesere, hii inaweza kuashiria ana ulemavu wa akili au usonji.

(b) *Kioo:* Hutumika kupima matamshi na uelewa ili kubainisha kama mwanafunzi anaweza kutambua sura yake na mwingine kama watakuwa zaidi ya mmoja kwenye kioo.

#### Namna ya kutumia kioo

Mwanafunzi anatumia kioo kujiangalia na kufanya vitendo kama kugusa pua yake kwenye kioo au kugusa vidole vya mikono. Tathmini inafanyika kupima jinsi mwanafunzi anavyoitikia na kama anaweza kutambua sura yake. Mwanafunzi akishindwa kutambua sura yake inayoonekana kwenye kioo inaweza kuashiria ulemavu wa akili au usonji.

FOR ONLINE READING ONLY

(c) ***Kibao fumbo:*** Hiki ni kibao chenye namba, herufi au maumbo mbalimbali. Hutumika kupima utambuzi wa namba, herufi au maumbo.

### Namna ya kutumia kibao fumbo

Mchakato huu unahusisha mwanafunzi kutumia kibao fumbo kinachofaa kwa umri wake. Kibaofumbo kina vipande vikubwa ambavyo vina sura au picha rahisi. Lengo la zoezi hili ni kuweka vipande vya fumbo sehemu zinazofaa ili kutengeneza picha nzima. Kufanya tathmini ili kuona namna mwanafunzi anavyokabiliana na zoezi. Mwanafunzi akishindwa kuweka vipande kwa usahihi, kukosa uvumilivu, au kutoweza kuelewa kazi kwa ujumla kunaweza kuashiria ulemavu wa akili au usonji.

## Kazi ya kufanya 2.6

Wakati wa mchakato wa ufundishaji darasani umegundua kuwa mwanafunzi mmoja anachagamoto ya mawasiliano, hawezi kutembea vizuri na ana matatizo mengine ya kimwili. Kwa kutumia maktaba na vyanzo rasmi vya mtandaoni eleza zana utakazozitumia katika ubainishaji wa awali wa changamoto za mwanafunzi huyo. Andika dondoo kwa njia ya programu andishi kisha hifadhi kwenye mkoba wa kazi.

## Zoezi la 2.6

Kama mtaalamu wa elimu jumuishi, eleza namna utakavyotumia zana mbalimbali kumtambua mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na usonji.

## Zoezi la marudio

1. Umegundua mwanafunzi wako mmoja anashindwa kuelezea jambo alilojifunza kipindi kilichopita. Fafanua mbinu unayoweza kuitumia kumsaidia mwanafunzi huyo kujifunza kwa ufasaha akiwa darasani.
2. Baada ya kujifunza ubainishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, umegundua kuwa hasira, huzuni au kujitenga ni moja ya viashiria vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Eleza aina ya ulemavu walionao na jinsi utakavyoweza kuwasadia wanafunzi wenye changamoto hizo.
3. Ushirikiano kati ya waelimishaji, wazazi, na wataalamu ni muhimu katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanajifunza kikamilifu. Kama mwalimu mahiri, eleza majukumu ya kila mdau anavyoweza kutekeleza elimu jumuishi na kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanapata mahitaji husika.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Tatu

# Utoaji wa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu

## Utangulizi

*Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji katika darasa jumuishi unapaswa kuwatambua wanafunzi wenye mahitaji maalumu na kuwapatia afua stahiki. Katika sura hii, utajifunza dhana ya afua stahiki, mbinu za utoaji wa afua stahiki na changamoto zinazojitokeza katika kutoa afua stahiki. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutoa afua stahiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.*

## Fikiri

Nyenzo muhimu katika utoaji wa elimu jumuishi

### Dhana ya afua stahiki

Afua stahiki ni huduma inayotolewa kwa watu wenye mahitaji maalumu. Mchakato huu, unashughulikia kutatua changamoto. Vilevile, huduma hizi zinamsaidia mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kuongeza ufanisi katika ujifunzaji na kukuza uwezo wa kujitegemea. Hivyo, afua stahiki inaweza kuwa ya kielimu, kisaikolojia, au kiafya kulingana na mahitaji.

Afua stahiki zinaweza kuboresha miundombinu ya shule kama vile madarasa, vyoo, matumizi ya vifaa jumuishi vya kufundishia na kujifunzia na kuwepo kwa walimu mahiri wa kutoa taaluma stahiki kwa kila mwanafunzi. Vilevile, kufanya ufuatiliaji na kutathmini maendeleo ya mwanafunzi katika ujifunzaji na kutoa mrejesho kwa familia na jamii ili kushirikiana katika kutoa afua stahiki.

### Aina za afua stahiki

Afua stahiki zinaweza kugawanyika kulingana na aina za mahitaji aliyonayo mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu. Afua hizi ni kama zifuatavyo:

***Afua stahiki za kielimu:*** Ni hatua na mikakati inayowekwa ili kuhakikisha kwamba mazingira ya ujifunzaji yanakuwa wezeshi kwa maendeleo ya mwanafunzi. Zifuatazo ni afua stahiki za kielimu:

FOR ONLINE READING ONLY

(a) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ambayo yanazingatia ulinzi na usalama wa mwanafunzi ndani na nje ya darasa. Miundombinu rafiki na fikivu itawezesha mwanafunzi kufika eneo husika kwa urahisi, mfano: darasani, maliwato, bwaloni na viwanja vya michezo;

(b) Kutumia zana na mbinu shirikishi darasani kama vile nyimbo, michezo, maigizo kwa kuzingatia mahitaji ya kila mwanafunzi. Vilevile, kutumia vifaa vya TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji kama simu janja, tabuleti, video ze nye tafsiri ya maandishi na picha ili kufanikisha ujifunzaji unaojumuisha mawasiliano ya kielektroniki;

(c) Kutoa motisha kwa kila mwanafunzi ili kuchochea ujifunzaji wake darasani;

(d) Kusisitiza matumizi ya maandishi makubwa, Braille, lugha ya alama na pichamguso;

(e) Kuongeza muda wakati wa kufanya mtihani; na

(f) kukuza utamaduni jumuishi shuleni, mfano kusisitiza ushirikiano kati ya wanafunzi, ushirikishwaji wa uongozi darasani na ufundishaji rika.

***Afua stahiki za kiafya:*** Ni mikakati inayofuatwa ili kuhakikisha afya na usalama wa mwanafunzi shuleni na nyumbani unakuwa bora. Zifuatazo ni afua stahiki za kiafya:

(a) Uchunguzi wa Afya ni muhimu ili kubaini magonjwa ya mapema na kuchukua hatua za matibabu. Hii itahusisha ufuatiliaji wa historia ya kiafya ya mwanafunzi;

(b) Kutoa huduma za kinga kwa mwanafunzi ili kuzuia magonjwa ya kuambukiza. Mfano wa kinga zinazotolewa shuleni ni pamoja na magonjwa ya mlipuko, kichocho na minyoo; na

(c) Kufanya usafi wa mazingira kwenye maeneo ya shule na nyumbani ili kuzuia maambukizi na magonjwa yasiyo ya lazima kwa wanafunzi wote. Vilevile, usafi wa vyombo vya chakula, uhifadhi wa chakula na maji safi ni muhimu kwa ustawi na afya ya mwanafunzi.

***Afua stahiki za kijamii:*** Ni huduma inayotekelezwa katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kila mwanafunzi kama vile kijamii, kidini, kiuchumi, kiutamaduni na kijinsia. Afua hii inakusudia kupunguza au kuondoa ubaguzi na kuongeza fursa za usawa kwa wanafunzi wote. Zifuatazo ni afua stahiki za kijamii:

(a) Kutekeleza elimu jumuishi shuleni na kutoa fursa kwa kila mwanafunzi katika ujifunzaji;

(b) Utoaji wa huduma za afya kwa lengo la kuondoa ubaguzi na kuhakikisha kuwa huduma za afya zinapatikana na zinawafikia wanafunzi wote. Mfano, kuwepo kwa zahanati ya shule, sanduku la huduma ya kwanza na utoaji wa elimu ya afya;

FOR ONLINE READING ONLY

(c) Kuwa na miundombinu jumuishi ili kusaidia katika ufundishaji na ujifunzaji. Hii itahusisha kuwepo kwa majengo yanayofikika kirahisi mfano madarasa, vyoo vya kawaida na vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu na matumizi ya vifaa vya ujifunzaji vinavyozingatia mahitaji ya mwanafunzi;

(d) Ushirikishaji wa wazazi au walezi kwenye ujifunzaji wa mwanafunzi; na

(e) Ushiriki wa jamii kwenye upatikanaji na maendeleo ya elimu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu.

### Kazi ya kufanya 3.1

Tumia maktaba na vyanzo rasmi vya taarifa kuchambua jinsi aina mbalimbali za afua stahiki zinavyosaidia ujifunzaji wa mwanafunzi wenye mahitaji maalumu. Hifadhi kazi yako kwenye mkoba wa kazi.

### Zoezi la 3.1

1. Kazi mojawapo ya mtaalamu wa elimu jumuishi ni kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu. Eleza aina za afua stahiki anazopaswa kutoa kwa mwanafunzi mwenye changamoto za kitabia.
2. Wakati wa ufundishaji na ujifunzaji umegundua kuwa mwanafunzi mmoja huwa anasogeza kitabu karibu na uso wake wakati wa kusoma. Eleza afua stahiki za kielimu utakazompa mwanafunzi huyo.

## Umuhimu wa kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu

Kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anapata fursa ya kujifunza kwa njia inayomfaa. Wanafunzi wenye mahitaji maalumu mara nyingi hukabiliwa na changamoto ambazo zinaweza kuathiri uwezo wao wa kuelewa na kushiriki katika mchakato wa kujifunza. Hivyo basi, kutoa afua stahiki ni hatua ya msingi katika kuwatengenezea mazingira bora ya ujifunzaji ili kuhakikisha kuwa wanapata elimu inayowawezesha kufaulu na kujiendeleza katika maisha yao. Utoaji wa afua stahiki kwa wanafunzi hawa katika ujifunzaji ni muhimu kwa sababu zifuatazo:

(a) Kuwezesha ujifunzaji: Afua stahiki husaidia mwanafunzi kuelewa na kujifunza kwa ufanisi zaidi, kwani zinazingatia mahitaji yake maalumu kupitia programu mbalimbali za kielimu;

(b) Kuongeza usawa: Afua stahiki husaidia kuondoa vikwazo vinavyoweza kuathiri uwezo wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kushiriki kikamilifu katika

FOR ONLINE READING ONLY

(c) Kuwa na miundombinu jumuishi ili kusaidia katika ufundishaji na ujifunzaji. Hii itahusisha kuwepo kwa majengo yanayofikika kirahisi mfano madarasa, vyoo vya kawaida na vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu na matumizi ya vifaa vya ujifunzaji vinavyozingatia mahitaji ya mwanafunzi;

(d) Ushirikishaji wa wazazi au walezi kwenye ujifunzaji wa mwanafunzi; na

(e) Ushiriki wa jamii kwenye upatikanaji na maendeleo ya elimu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu.

### Kazi ya kufanya 3.1

Tumia maktaba na vyanzo rasmi vya taarifa kuchambua jinsi aina mbalimbali za afua stahiki zinavyosaidia ujifunzaji wa mwanafunzi wenye mahitaji maalumu. Hifadhi kazi yako kwenye mkoba wa kazi.

### Zoezi la 3.1

1. Kazi mojawapo ya mtaalamu wa elimu jumuishi ni kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu. Eleza aina za afua stahiki anazopaswa kutoa kwa mwanafunzi mwenye changamoto za kitabia.
2. Wakati wa ufundishaji na ujifunzaji umegundua kuwa mwanafunzi mmoja huwa anasogeza kitabu karibu na uso wake wakati wa kusoma. Eleza afua stahiki za kielimu utakazompa mwanafunzi huyo.

## Umuhimu wa kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu

Kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anapata fursa ya kujifunza kwa njia inayomfaa. Wanafunzi wenye mahitaji maalumu mara nyingi hukabiliwa na changamoto ambazo zinaweza kuathiri uwezo wao wa kuelewa na kushiriki katika mchakato wa kujifunza. Hivyo basi, kutoa afua stahiki ni hatua ya msingi katika kuwatengenezea mazingira bora ya ujifunzaji ili kuhakikisha kuwa wanapata elimu inayowawezesha kufaulu na kujiendeleza katika maisha yao. Utoaji wa afua stahiki kwa wanafunzi hawa katika ujifunzaji ni muhimu kwa sababu zifuatazo:

(a) Kuwezesha ujifunzaji: Afua stahiki husaidia mwanafunzi kuelewa na kujifunza kwa ufanisi zaidi, kwani zinazingatia mahitaji yake maalumu kupitia programu mbalimbali za kielimu;

(b) Kuongeza usawa: Afua stahiki husaidia kuondoa vikwazo vinavyoweza kuathiri uwezo wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kushiriki kikamilifu katika

FOR ONLINE READING ONLY

ujifunzaji. Kwa hiyo, mazingira ya kujifunza yanakuwa na usawa, ambapo kila mwanafunzi anapata nafasi sawa ya kuonyesha uwezo wake;

(c) *Kujenga kujiamini:* Mwanafunzi anapopewa afua stahiki, anapata fursa ya kukabiliana na changamoto katika mazingira yake, hivyo humjengea hali ya kujiamini na kutambua uwezo wake katika kushiriki shughuli za ujifunzaji;

(d) *Kukuza ushirikiano:* Afua hizi zinampa mwanafunzi fursa ya kushiriki katika shughuli za kikundi, ambapo anaweza kujifunza stadi za ushirikiano, uongozi, na mawasiliano. Stadi hizi zitamjengea uhusiano mzuri na wenzake, kukuza uelewano, na kujifunza kutoka kwa kila mmoja; na

(e) *Upatikanaji wa zana stahiki:* Zana hizi ni muhimu kwa sababu zinamsaidia mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kujifunza kwa ufanisi. Zana hizi zinamwezesha mwalimu kukabiliana na changamoto ambazo mwanafunzi anakumbana nazo, na hivyo kuimarisha mazingira ya kujifunza na kupelekea mwanafunzi kukuza uwezo wake wa kimasomo.

Kutoa afua stahiki ni muhimu katika kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanapata elimu bora. Hii inawasaidia kufikia malengo yao na kujenga jamii inayowajali na kuwasaidia wote.

## Mbinu za utoaji wa afua stahiki

Hii ni namna ya kutoa ushauri, huduma na suluhisho la changamoto mbalimbali katika ujifunzaji kwa wanafunzi wote ndani na nje ya darasa. Zifuatazo ni mbinu za kutoa afua stahiki:

(a) Kutengeneza mpango binafsi wa ufundishaji ambao unamsaidia mwanafunzi kukidhi mahitaji ya msingi;

(b) Kutoa ushauri na unasihi ambao husaidia kusimamia tabia na mienendo ya mwanafunzi darasani. Hii inapunguza unyanyapaa na utegemezi kwa kuwezesha mazingira rafiki ya ufundishaji na ujifunzaji;

(c) Ushirikishwaji darasani ambao unamsadia mwanafunzi kushiriki kikamilifu katika majadiliano, uwasilishaji na shughuli zote za ujifunzaji;

(d) Kualika mgeni, kutoa motisha na mafunzo. Mbinu hii, inasaidia mwanafunzi kujenga uwezo wa kujithamini na kuthaminiwa;

(e) Kutumia michezo kama mbinu changamshi, ambayo husaidia kuimarisha misuli midogo na mikubwa, kufanya uchechemuzi wa akili, kutanua mapafu na kuleta msawazo; na

(f) Kutoa huduma muhimu shuleni ikiwemo mpango wa chakula, maji safi na salama na vyoo stahiki.

FOR ONLINE READING ONLY

(g) Kufanya tathmini endelevu ambayo inahusisha kufuatilia maendeleo na mahitaji ya ujifunzaji wa mwanafunzi. Hii inaweza kujumuisha tathmini ya kielimu na kiafya;

### Kazi ya kufanya 3.2

Tumia makala mbalimbali kutoka maktaba na vyanzo rasmi vya taarifa, andika dondoo za namna unavyoweza kutumia mbinu za kutoa afua stahiki kwa wanafunzi wenye changamoto za kijamii, kitabia na kihisia. Hifadhi dondoo katika mkoba wa kazi.

### Zoezi la 3.2

1. Kuna mbinu mbalimbali za utoaji wa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu. Fafanua changamoto zinazoweza kujitokeza wakati wa kuzitumia mbinu hizo na namna ya kuzitatua.
2. Umegundua kwamba katika darasa unalofundisha kuna mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili. Eleza mbinu utakazotumia kutoa afua stahiki ili mwanafunzi huyo aweze kujifunza vizuri.

### Kazimradi 3.1

Soma makala mbalimbali kutoka maktaba na vyanzo rasmi vya taarifa, tafuta rejea zinazofafanua kuhusu afua stahiki. Eleza namna afua stahiki zinavyotekelezwa chuoni kwako. Andika taarifa ukizingatia afua stahiki za kielimu, kiafya na kijamii. Kisha hifadhi kwenye mkoba wako wa kazi.

## Afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu

Katika mazingira ya elimu jumuishi ni muhimu kutambua na kushughulikia mahitaji maalumu ya mwanafunzi ili kuhakikisha kila mmoja anapata fursa sawa ya kujifunza. Mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu, kama vile mwenye uziwi, uoni, ualbino, ulemavu wa akili, usonji,viungo na wale wanaoishi katika mazingira hatarishi, wanahitaji afua stahiki zinazoendana na mahitaji yao. Kwa kutoa afua stahiki, itasaidia mwanafunzi huyo kupata mazingira sahihi yanayowezesha ujifunzaji. Zifuatazo ni afua stahiki kwa kila kundi la wanafunzi wenye mahitaji maalumu:

### Afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye uziwi

Mwanafunzi aliyebainika kuwa na changamoto ya uziwi hushindwa kufikia malengo yake ya kielimu na kijamii. Ili aweze kushiriki kikamilifu katika kujifunza, mwalimu

FOR ONLINE READING ONLY

anapaswa kuzingatia afua stahiki zifuatazo:

(a) Matumizi ya zana zinazoonekana kama vile picha au vitu halisi, video zenye picha na maandishi wakati wa kutoa maelekezo ya ujifunzaji;

(b) Kuhakikisha kuwa madarasa yana mazingira bora kwa mwanafunzi mwenye uziwi kama vile mwanga wa kutosha ili mwanafunzi aweze kusoma mdomo wa mwalimu anapozungumza na kuhakikisha hakuna kelele nyingi darasani zinazoweza kumvuruga mwanafunzi;

(c) Kutoa vifaa vya kukuza usikivu vilivyoboreshwa, mfano shime sikio kulingana na kiwango chake cha baki ya usikivu. Kifaa hicho kinaweza kumsaidia mwanafunzi kusikia maelezo kutoka kwa walimu na wanafunzi wenzake;

(d) Kuanzisha programu za kujifunza lugha ya alama kwa wanafunzi wote, walimu na jamii ili kuboresha mawasiliano;

(e) Inashauriwa mkao katika darasa jumuishi uwe nusu duara au mwanafunzi mwenye uziwi akae mbele ya darasa ili aweze kumuona mwalimu au mkalimani wa lugha ya alama pindi maelekezo yanapotolewa;

(f) Huduma za kisaikolojia na kijamii kwa mwanafunzi mwenye uziwi zinahitajika ili kumsaidia kushughulikia changamoto za kihisia ambazo zinaweza kutokea kutokana na hali yake; na

(g) Kutoa ushauri kwa wazazi/walezi pale mwanafunzi mwenye uziwi anapogundulika anahitaji rufaa ya kimatibabu.

### Afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni

Mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni anaweza kujifunza kwa ufanisi licha ya changamoto za kutoona au kuona kwa shida. Hivyo, ili aweze kujifunza kwa ufanisi vifaa, mbinu za kufundishia na kujifunzia, huduma za kijamii na kisaikolojia zinahitajika. Zifuatazo ni afua stahiki zinazohitajika kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.

(a) Katika kukaa darasani, umbali kati ya mwanafunzi na ubao uzingatiwe kwa mujibu wa mahitaji ya mwanafunzi mwenyewe pamoja na matumizi ya vikuza maandishi;

(b) Mwalimu amshauri mzazi kumpeleka mwanafunzi kwenye matibabu stahiki;

(c) Kuwepo kwa walimu wenye ujuzi wa Braille ili kumfundisha mwanafunzi kutumia maandishi haya na kumsaidia kufuatilia masomo yake;

(d) Vifaa vya kielimu, mfano kibao henamu na mashine za Braille ambavyo vinaweza kubadilisha nukuu za somo na mitihani vinatakiwa vitumiwe na mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni katika ujifunzaji. Vitabu na machapisho

FOR ONLINE READING ONLY

yote yanatakiwa kutafsiriwa kwa maandishi ya Braille au maandishi yaliyokuzwa kwa mwanafunzi mwenye uoni hafifu;

(e) Mwanafunzi achangamane na wenzake wakati wa ujifunzaji ili kuondoa hali ya kujitenga;

(f) Mwanafunzi apewe muda wa kutosha wa kufanya kazi anazopangiwa ukilinganisha na wale wasio na mahitaji maalumu;

(g) Mwalimu anatakiwa kutumia mbinu mbadala za kufundishia kama vile maelezo ya maneno, vielelezo vya kugusa, na majaribio ya kihisia;

(h) Huduma za ushauri nasaha ni muhimu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni ili kumsaidia kukabiliana na changamoto za kisaikolojia na kijamii zinazoweza kutokea kutokana na hali yake. Aidha, ushauri wa kitabibu ni muhimu kwa mwanafunzi mwenye changamoto ya uoni;

(i) Mazingira ya nje na ndani ya darasa yanapaswa kuboreshwa ili kumwezesha mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kutembea bila kikwazo; na

(j) Mwanafunzi afundishwe maandishi ya Braille, teknolojia saidizi na apewe mafunzo kabilishi ya ujongeaji.

### Afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ualbino

Afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ualbino ni muhimu ili kuhakikisha mazingira bora ya kujifunzia na kusaidia kuepuka changamoto zinazotokana na hali ya kiafya. Zifuatazo ni afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ualbino:

(a) Mara nyingi mwanafunzi mwenye ualbino hukabiliwa na matatizo ya kuona. Hivyo, vifaa vinavyoweza kumsaidia ni kama vile miwani ya kupunguza mwanga wa jua;

(b) Inashauriwa mwanafunzi kukaa karibu na ubao ili aweze kuona vizuri. Pia, anaweza kutumia vifaa vya kielektroniki vinavyoweza kumsaidia kukuza maandishi au picha;

(c) Anapaswa kutumia mafuta ya kuzuia mionzi ya jua, kofia pana, miwani ya jua, na mavazi yanayofunika sehemu kubwa ya mwili ili kuzuia uharibifu wa ngozi kutoka kwenye jua kali; na

(d) Anaweza kukabiliwa na changamoto za kijamii kama vile ubaguzi au kunyanyapaliwa. Ushauri wa kisaikolojia na msaada wa kijamii ni muhimu ili kujenga kujiamini na kukabiliana na hali hiyo.

### Afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili

Mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili anahitaji afua stahiki ambazo zitamsaidia kuboresha ujifunzaji, ustawi wa kijamii na afya ya kisaikolojia. Zifuatazo ni afua

FOR ONLINE READING ONLY

stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili:

(a) Inashauriwa kuwa na mpango binafsi wa kielimu ambao umebainishwa kulingana na mahitaji ya mwanafunzi. Mpango huu unapaswa kutekelezwa kwa kushirikiana na walimu, wazazi na wataalamu wa elimu maalumu;

(b) Mwalimu anashauriwa kutumia mbinu za kufundishia ambazo ni shirikishi na zinazohusisha mazoezi ya mara kwa mara, na kuimarisha ustadi wa kijamii na kiakili;

(c) Matumizi ya vifaa stahiki humjengea uwezo wa kuchechemua milango ya fahamu, kufahamu mambo, kutofautisha vitu kwa ukubwa, rangi, umbile na kupanga kwa usahihi;

(d) Mwalimu anashauriwa kutoa maelekezo machache na kutumia vitendo zaidi ili mwanafunzi aweze kufanya vitendo vinavyochochea uchangamshi wa awali wa usikivu kama vile kuwasha na kuzima redio;

(e) Mwanafunzi afundishwe stadi za maisha mfano usafi, mwenendo na tabia inayokubalika ili aweze kukubalika kushiriki katika matendo mbalimbali na wanafunzi wenzake na jamii inayomzunguka; na

(f) Mwanafunzi anaweza kuwa na mahitaji maalumu ya kiafya yanayohitaji ufuatiliaji wa mara kwa mara kama vile matibabu ya kisaikolojia na dawa za kuboresha utendaji wa akili.

### Afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye usonji

Mwanafunzi mwenye ulemavu wa usonji ana upekee wake, hivyo ni muhimu kuhakikisha kuwa afua stahiki zinatolewa kwa kuzingatia mahitaji binafsi ya mwanafunzi husika. Zifuatazo ni afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa usonji:

(a) Mazingira ya darasani yanapaswa kuwa na utulivu, bila kelele au msongamano mwingi, ili kuepuka kumchosha au kumsumbua mwanafunzi huyo. Mwanafunzi anaweza kuwa na hisia kali kwa mwanga, sauti, au harufu, hivyo mazingira ya darasa yanapaswa kuzingatia hilo ili kuamsha milango ya fahamu ya kujifunzia;

(b) Matumizi ya mbinu mbadala za mawasiliano kama vile picha, lugha ya ishara au teknolojia ya mawasiliano zitamsaidia kushiriki kwenye makundi wakati wa kujifunza;

(c) Kuwe na mpango maalumu wa ujifunzaji kwa kila mwanafunzi ambao unazingatia malengo na changamoto binafsi za ujifunzaji wake. Mpango huu unasaidia kutoa mwelekeo wa jinsi mwanafunzi atakavyosaidiwa katika masomo yake na katika maendeleo yake ya jumla;

FOR ONLINE READING ONLY

(d) Kutumia picha na zana halisi za ufundishaji na ujifunzaji ambazo humjengea uwezo wa kutofautisha vitu kwa ukubwa, rangi, umbile na kupanga kwa usahihi;

(e) Kutoa motisha kwa mwanafunzi ambayo itamjengea stadi za mawasiliano, umakini, mjongeo na ushirikiano. Hivyo, mpongeze mwanafunzi kwa kila hatua anayofanikiwa wakati wa ujifunzaji; na

(f) Mwalimu anatakiwa kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu usonji na namna ya kumfundisha mwanafunzi mwenye usonji. Hii inajumuisha kutumia mbinu za kufundishia ambazo zinaendana na mahitaji yake ya kujifunza, kama vile bango la maneno, mahema yenye majina mbalimbali, video na vitendo.

### Afua stahiki kwa mwanafunzi anayeishi kwenye mazingira hatarishi

Kumsaidia mwanafunzi anayeishi kwenye mazingira hatarishi kunalenga kuondoa vizuizi au changamoto za kijamii, kifedha, na kisaikolojia zinazoweza kuathiri elimu yake. Zifuatazo ni afua stahiki za mwanafunzi anayeishi katika mazingira hatarishi:

(a) Kutoa vifaa vya shule kama vile vitabu, sare, kompyuta, tabuleti, na vifaa vingine vya michezo kwa mwanafunzi ili kuhakikisha kuwa anahudhuria shuleni;

(b) Kutoa chakula cha mchana shuleni kwa wanafunzi wenye mazingira magumu ili kusaidia kuboresha afya zao na uwezo wao wa kujifunza;

(c) Kutoa huduma za ushauri nasaha kwa mwanafunzi ili kumsaidia kukabiliana na matatizo ya kisaikolojia na kihisia kutokana na mazingira yake;

(d) Kushirikiana na mashirika ya kijamii kusaidia mahitaji ya msingi kama malazi na mavazi;

(e) Upatikanaji wa walimu wa ziada au wakufunzi wanaoweza kumsaidia mwanafunzi aliye na changamoto katika ujifunzaji; na

(f) Kuwepo kwa sera zinazowalinda watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na kuhakikisha kuwa zinatekelezwa ili wasikose fursa ya kupata elimu.

FOR ONLINE READING ONLY

### Kazi ya kufanya 3.3

Kwa kutumia vyanzo rasmi vya taarifa ainisha jinsi utakavyotoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye changamoto uoni. Eleza ni kwa namna gani mwanafunzi huyo atanufaika na huduma hiyo. Hifadhi kazi kwenye kabrasha la elimu jumuishi

## Zoezi la 3.3

1. Wapo wanajamii wenye mitazamo hasi kuhusu sababu za ulemavu. Ukiwa kama mtaalamu wa elimu jumuishi, bainisha mitazamo hiyo kwa hoja zisizopungua tano. Kisha eleza ni kwa namna gani unaweza kurekebisha mitazamo hiyo.

2. Mwalimu wa elimu jumuishi anao uwezo wa kubaini changamoto za ujifunzaji kwa mwanafunzi wenye uziwi. Wewe kama mdau wa elimu jumuishi, ainisha afua stahiki zisizopungua tano kwa mwanafunzi mwenye changamoto ya uziwi.

3. Kufikia malengo ya elimu jumuishi, utoaji wa afua stahiki umewekewa msisitizo kwa wanafunzi wanaoishi kwenye mazingira hatarishi. Bainisha makundi yasiyopungua manne ya wanafunzi wanaoishi katika mazingira hatarishi kisha fafanua afua stahiki zinazoweza kutolewa kwa wanafunzi hao.

FOR ONLINE READING ONLY

### Changamoto katika utoaji wa afua stahiki

Utoaji wa afua stahiki katika elimu jumuishi una changamoto nyingi ambazo huathiri ujifunzaji wa mwanafunzi. Zifuatazo ni changamoto katika utoaji wa afua stahiki:

(a) Upatikanaji wa rasilimali na utoaji wa afua stahiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu unahitaji rasilimali watu, vifaa na fedha. Vyote hivyo ni gharama kubwa, ukosefu wa rasilimali hiyo husababisha malengo ya utoaji wa afua stahiki kwa wanfunzi wenye mahitaji maalumu kutofikiwa. Hivyo, ni muhimu kuwekeza rasilimali za kutosha katika eneo hili ili kufikia malengo ya utoaji wa elimu jumuishi;

(b) Ushiriki mdogo wa wadau katika utoaji wa afua stahiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu mfano ushiriki hafifu wa wazazi, walezi, jamii, mashirika yasiyo ya kiserikali na taifa kwa ujumla husababisha wanafunzi kukosa msaada unaohitajika katika ujifunzaji. Ni muhimu wadau kushiriki kikamilifu katika kutoa afua stahiki, kufanya tathmini na kutoa mrejesho wa pamoja;

(c) Mtazamo hasi kutoka kwenye jamii kuhusu watu wenye mahitaji maalumu. Hii husababisha kutengwa na jamii kutokana na changamoto walizonazo mfano mtoto mwenye ulemavu wa viungo au akili anaweza kukosa fursa ya kupata elimu. Ni muhimu kutoa elimu kwa jamii ili isiwatenge watu wenye mahitaji maalumu; na

(d) Miundombinu isiyo rafiki na fikivu kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalum. Kwa mfano ukosefu wa vyoo maalumu vinavyozingatia ujumuishi na vifaa saidizi vya kujifunzia. Hivyo, ni muhimu kuboresha miundombinu iwe rafiki na fikivu kwa wanafunzi wote ili waweze kujifunza kwa ufasaha.

## Kazi ya kufanya 3.4

Tembelea shule ya jirani, fanya mahojiano na uongozi wa shule kuhusu changamoto za utoaji wa afua stahiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu shuleni. Kisha andika changamoto hizo na namna zinavyotatuliwa. Hifadhi dondoo katika mkoba wa kazi.

## Zoezi la 3.4

1. Darasa jumuishi linajumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu na wasio na mahitaji maalumu. Eleza changamoto wanazokumbana nazo walimu katika kutoa afua stahiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
2. Ukiwa kama mtaalamu wa elimu jumuishi, eleza jinsi utakavyowaelimisha wazazi wa wanafunzi wenye uziwi kuondoa mitazamo hasi kwa watoto wao pale wanapotumia shime sikio kama afua stahiki.

## Zoezi la marudio

1. Walimu na walezi ni wadau muhimu katika utoaji wa afua stahiki kwa wanafunzi. Thibitisha kauli hiyo kwa hoja tano.
2. Mwalimu wa elimu jumuishi anao uwezo wa kutofautisha kati ya afua stahiki za kijamii na kiafya. Bainisha tofauti hizo.
3. Darasa jumuishi linajumuisha wanafunzi wenye changamoto za uoni. Eleza afua stahiki utakazotumia kuwawezesha kusoma katika darasa hilo.
4. Darasa jumuishi linajumuisha wanafunzi wenye vipaji na vipawa maalumu. Eleza namna unavyoweza kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye kipaji na mwenye kipawa cha pekee.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Nne

# Mbinu na zana za ufundishaji na ujifunzaji katika mazingira jumuishi

## Utangulizi

Mbinu na zana jumuishi zinahusisha milango ya fahamu zaidi ya mmoja ili kuchochea ari ya ujifunzaji kwa mwanafunzi. Vilevile, matumizi ya zana huenda sambamba na mbinu za kufundishia ili kusaidia katika kutatua changamoto na kuleta uhalisia katika ujifunzaji wa mwanafunzi. Katika sura hii, utajifunza mbinu za ujifunzaji katika darasa jumuishi, dhana ya zana za kufundishia na kujifunzia darasa jumuishi, na utengenezaji wa zana jumuishi. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia mbinu na zana stahiki katika darasa jumuishi na kukidhi mahitaji ya ujifunzaji.

## *Fikiri*

**Ufundishaji na ujifunzaji bila kuzingatia mbinu na zana jumuishi**

### Mbinu za ujifunzaji katika darasa jumuishi

Ni mikakati inayotumiwa kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu na wasio na mahitaji maalumu ili waweze kujifunza katika darasa jumuishi. Mbinu hizi huhakikisha kila mwanafunzi anajifunza kulingana na mahitaji yake binafsi. Mbinu za ujifunzaji kwenye darasa jumuishi humshirikisha mwanafunzi kuwa mtendaji katika ujifunzaji kwani ndio njia ya kukidhi mahitaji na huhusisha mlango wa fahamu zaidi ya mmoja. Jukumu la mwalimu ni kuwaongoza, kuwaelekeza au kuwaonesha namna ya kufanya shughuli mbalimbali kwa kutumia mbinu jumuishi na shirikishi darasani. Baadhi ya mbinu hizi ni:

(a) Ufundishaji wa pamoja: Katika mbinu hii walimu wawili au zaidi hufundisha darasani kila mmoja akitumia utaalamu wake kumsaidia mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu;

(b) Mwanafunzi kufundisha wanafunzi wenzake: Mbinu hii inatumiwa na mwanafunzi kwa kuchukua majukumu ya mwalimu kuelezea au kufafanua dhana fulani kwa wanafunzi wenzake; na

FOR ONLINE READING ONLY

(c) *Kutumia vifaa vya teknolojia:* Vifaa hivi husaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu ili waweze kufuatilia masomo yao. Kwa mfano; mashine za Braille, vinasa sauti, vifaa na programu zinazobadilisha maandishi kuwa matamshi, tabuleti, kompyuta, na simu janja.

Aidha, katika ufundishaji wa darasa jumuishi mbinu hizi zinaweza kuwezeshwa kikamilifu kwa kuhusisha ubunifu na unyumbufu katika kuzingatia mahitaji ya kila mwanafunzi na mitindo ya ujifunzaji. Hivyo, mbinu hizi zitakuwa fanisi kama zitahusisha matumizi ya njia nyingi za uwasilishaji, vitendo na ushirikishwaji.

## Faida za kutumia mbinu za ujifunzaji katika darasa jumuishi

(a) *Ushiriki wa wanafunzi wote:* Ni mbinu inayohakikisha kuwa wanafunzi wote wana nafasi ya kujifunza na kuonyesha ujuzi wao, bila kujali mahitaji yao ya kielimu, kijamii, au kiutamaduni. Inajenga mazingira ya usawa ambapo wanafunzi wote wanajihisi kuwa sehemu ya darasa;

(b) *Kuboresha ufanisi wa kila mwanafunzi:* Katika mbinu hii ujifunzaji ndani ya darasa jumuishi hutoa fursa kwa wanafunzi kujifunza kwa njia inayolingana na uwezo wao, vipaji, na mitindo yao ya kujifunza, kama vile kujifunza kwa kushirikiana, kujitegemea na kwa kutumia teknolojia saidizi. Hivyo, wanafunzi huongeza uelewa na kuwafanya waweze kujifunza kwa ufanisi zaidi;

(c) *Kuimarisha ujuzi na ushirikiano:* Kwa kutumia mbinu hii ujifunzaji katika darasa jumuishi huhimiza ushirikiano na mawasiliano kati ya mwanafunzi na mwanafunzi, mwanafunzi na mwalimu, na mwanafunzi na jamii. Hii husaidia kuendeleza ujuzi wa kielimu, kijamii na kuwafanya wanafunzi waweze kupata maarifa, kuishi pamoja, na kufanya kazi kwa ufanisi zaidi;

(d) *Kujifunza kwa usawa:* Ujifunzaji katika darasa jumuishi huhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaweza kufikia malengo yao ya kujifunza, bila kujali tofauti zao. Ujifunzaji huu huhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaweza kufanikiwa;

(e) *Kuongeza ari ya kujifunza:* Hutoa fursa kwa mwanafunzi kujifunza kwa urahisi kwa kuwa walimu hutumia mbinu mbalimbali zinazowafaa na kuwawezesha wanafunzi kujifunza kwa furaha zaidi; na

(f) *Hukuza kujitegemea na kujiamini:* Wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanapojumuishwa katika darasa jumuishi hujengewa kujiamini na kushiriki kujifunza pamoja na wenzao. Pia inawapa fursa ya kuwa huru zaidi katika kutatua changamoto na kuwa na mtazamo chanya.

FOR ONLINE READING ONLY

## Kazi ya kufanya 4.1

Umepewa uwezeshe mbinu ya masimulizi ambayo ni moja ya mbinu ya kufundishia kwenye madarasa jumuishi kwa darasa la Awali, la Kwanza, la Pili na la Tatu.

Andaa dondoo za kuwezesha namna ya kuitumia mbinu ya masimulizi, manufaa na tahadhari wakati wa kuitumia mbinu hiyo. Weka nukuu katika mkoba wa kazi.

## Zoezi la 4.1

1. Jiulize nini kitatokea kama utashindwa kutumia mbinu za ujifunzaji katika darasa jumuishi, kisha eleza faida za kutumia na hasara za kutotumia mbinu jumuishi katika ujifunzaji.
2. Mbinu shirikishi zinaweza kutumika katika ufundishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Eleza kwa mifano mbinu utakayotumia ili kuhakikisha inawashirikisha wanafunzi wote darasani.

## Dhana ya zana za kufundishia na kujifunzia darasa jumuishi

Zana za kufundishia na kujifunzia ni jumla ya vitu vyote anavyotumia mwalimu na mwanafunzi ili kurahisisha utendaji wa shughuli wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Kazi kubwa ya zana ni kumsaidia kila mwanafunzi katika utendaji wa shughuli na hatua za ujifunzaji. Miongoni mwa zana za msingi zinazotumika darasani ni rangi, vibao, picha, mchoro mguso na video zinazoonesha ujumuishi.

Aidha, zana ya ufundishaji na ujifunzaji ni kifaa au chombo kinachotumika kufanya kazi fulani. Hivyo zana katika darasa jumuishi, ni vielelezo au vitu vyote ambavyo vinaweza kutumika kuelezea dhana ya kitu kwa mwanafunzi wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Zana hizi jumuishi zinazingatia ukweli kwamba kila mwanafunzi ana njia yake ya ujifunzaji. Hivyo, ni muhimu kutafuta na kutumia zana rafiki ambazo zinahusisha mlango wa fahamu zaidi ya mmoja mfano; kuona, kusikia, kuhisi, kuonja na kunusa ili kuchochea ari ya ujifunzaji. Aidha, utengenezaji wa zana utazingatia mitindo ya ujifunzaji kama vile kuona, kusikia na kutenda kwa kuzingatia mahitaji ya kila mwanafunzi darasani.

## Aina za zana jumuishi

Zana zimegawanyika katika makundi makuu mawili:

(a) *Zana za asilia:* Ni zana rahisi ambazo hupatikana au kutengenezwa katika mazingira yanayomzunguka mwanafunzi kwa kutumia vitu halisi vilivyomo

FOR ONLINE READING ONLY

katika mazingira hayo. Mfano, matunda, mimea, mawe, mchanga na samani; na

(b) *Zana za kisasa:* Hizi ni zana ambazo ni ngeni na hazijazoeleka katika kuzitengeneza au kuzitumia. Mfano wa zana za kisasa ni; video, runinga, projekta, filamu, simu na kompyuta.

### Upatikanaji wa zana jumuishi

Mchakato wa upatikanaji wa zana jumuishi, unaweza kupatikana kwa njia ya kutengeneza, kufaragua na kununua. Aidha, katika upatikanaji wa zana za kufundishia na kujifunzia darasa jumuishi yafuatayo ni mambo ya kuzingatia:

(a) Urahisi wa upatikanaji wa zana yenyewe au makunzi na vifaa vitakavyotumika katika utengenezaji na ufaraguzi;

(b) Kuzingatia mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;

(c) Ubunifu katika kutengeneza au ufaraguzi wa zana; na

(d) Uwiano wa zana husika na mazingira ya darasa.

### Makundi ya zana jumuishi

Zana jumuishi za kufundishia na kujifunzia zimeainishwa katika makundi matatu yafuatayo:

(a) *Zana uoni:* Zana hizi zinahusiana na vitu vinavyo onekana kama vile michoro, chapa, mabango, ramani, tufe, vifani, vikaragosi, picha mguso, picha za kuchora, picha mnato, sinema bubu, ubao wa chaki, vitabu na makala mbalimbali.

(b) *Zana masikizi:* Hizi ni zana zinazohusisha kusikia sauti au milio mbalimbali kama vile ngoma, redio, kanda za redio, santuri, zomali, vuvuzela, filimbi na vinasa sauti.

(c) *Zana uoni-masikizi:* Hizi ni zana zinazohusiana na kusikia na kuona kwa wakati mmoja. Kwa mfano, runinga, video, kanda za video, santuri, filamu, simu janja, tabuleti, kompyuta na sinema zenye kutoa sauti na kuonesha picha.

### Kazi ya kufanya 4.2

Tembelea karakana/chumba cha kuhifadhia zana za kufundishia na kujifunzia, zichunguze na kuzipanga kulingana na aina yake. Kisha fafanua sifa stahiki za zana za kufundishia na kujifunzia darasa jumuishi. Tumia maktaba na vyanzo rasmi mtandaoni kupata maarifa zaidi.

FOR ONLINE READING ONLY

## Zoezi la 4.2

1. Katika kazi za vikundi darasani, kundi lako limechaguliwa kueleza makundi ya zana za kufundishia na kujifunzia darasa jumuishi. Eleza kwa mifano zana za uoni-maskizi kwa mwanafunzi mwenye uoni hafifu.
2. Kwa kutumia utaalamu ulionao eleza kwa mifano matumizi ya zana uoni kwa mwanafunzi mwenye changamoto ya uziwi.

### Utengenezaji wa zana jumuishi

Huu ni mchakato wa kuunda zana au kifaa kwa kutumia makunzi yaliyopo katika mazingira yanayomzunguka mwanafunzi ili kujenga dhana ya kitu anachofundishwa kwa urahisi. Aidha, baadhi ya vifaa vinaweza kufaraguliwa na kuwa zana za kufundishia ili kuleta uhalisia wa ujifunzaji kulingana na umahiri uliokusudiwa. Ufaraguzi huu unaweza kuhusisha vitu kama vile madirisha, meza au viti vilivyopo darasani kama zana za kufundishia maumbo mbalimbali katika somo mfano somo la Hisabati. Vilevile, unaweza kutumia ubao wa kuandikia darasani ili kufundishia utambuzi wa rangi au umbo la pembe nne.

Zana ambazo zinaweza kutumika kufundishia na kujifunzia katika darasa jumuishi ni pamoja na kibao fumbo, bao, karata, dadu, domino, chati za michezo, drafti, vihesabio na midoli, kadi za herufi/maneno/sentensi, kadi za namba, kadi za picha, vipande vya mbao, vifani vya kanda za video, runinga na redio. Zana nyingine ni michoro, picha, filimbi, kengele, ngoma, zeze, kinanda, viongeza sauti, vikuza maandishi, zana mguso, kamusi ya Lugha ya Alama ya Tanzania, na chati ya alfabeti za lugha ya alama ya Tanzania.

## Kazi ya kufanya 4.3

Chagua somo unalofundisha na tafuta shughuli moja ya ujifunzaji, andaa makunzi na vifaa vya kutengeneza zana mbili jumuishi. Kisha, tengeneza zana hizo kwa kuzingatia hatua za utengenezaji wa zana. Hifadhi zana zako katika chumba cha zana.

## Zoezi la 4.3

1. Hatua za ufaraguzi na utengenezaji wa zana huweza kutofautiana au kufanana kutegemeana na kifaa kinachokusudiwa kuundwa. Eleza hatua unazopaswa kuzifuata unapofaragua zana za kufinyanga zitakazotumika katika darasa jumuishi.
2. Eleza umuhimu wa zana jumuishi katika ufundishaji na ujifunzaji ukihusianisha na stadi za karne ya 21.

FOR ONLINE READING ONLY

3. Kwa kutumia teknolojia na vyanzo rasmi mtandaoni tengeneza zana ambayo inaweza kutumiwa na wanafunzi wenye mahitaji maalumu kisha eleza namna utakavyoitumia darasani.
4. Chagua shughuli moja katika umahiri pendekezwa wa ujifunzaji darasa la pili, kisha tengeneza zana tatu zinazozingatia ujumuishi katika ujifunzaji.

## Kazimradi 4.1

Chunguza zana za mfano zilizopo katika chumba cha kuhifadhia zana, chagua zana tano kisha zielezee kwa kuandika yafuatayo;

1. Taja jina la zana husika.
2. Taja makunzi yaliyotumika kutengenezea zana hiyo.
3. Orodhesha hatua za utengenezaji zana hiyo.
4. Bainisha mchango wa zana husika katika ujifunzaji wa darasa jumuishi.
5. Eleza matumizi ya zana husika kwa maendeleo ya mwanafunzi katika ujifunzaji.

## Zoezi la marudio

1. Mwanafunzi anafurahia na kulipenda somo kulingana na mbinu zilizotumika darasani ambazo zimeweza kumsaidia kutatua changamoto zake za ujifunzaji. Eleza umuhimu wa kutumia mbinu sahihi za ujifunzaji katika mazingira jumuishi.
2. Umepewa darasa la tatu ufundishe somo la uraia na maadili, ukagundua wanafunzi wana mwitikio hasi katika mbinu uliyotumia ambayo sio shirikishi kwao. Ukiwa kama mtaalamu eleza kwa mifano mbinu utakazotumia ili wanafunzi waweze kuwa na mwitikio chanya.
3. Chagua shughuli moja ya ufundishaji katika umahiri au somo husika. Kisha, eleza mbinu utakazozitumia ukionesha faida na changamoto zake katika darasa jumuishi.
4. Serikali imekuajiri kama mwalimu mahiri na unauwezo mkubwa wa kufundisha darasa jumuishi. Je utatumia zana zipi katika kumwezesha mwanafunzi mwenye uoni hafifu kujifunza darasani ?
5. Zipo faida za kutumia zana jumuishi kwa sababu kila mwanafunzi ana namna anavyojifunza kulingana na mahitaji yake. Wapo wanafunzi wanaojifunza vizuri kwa kuona, wengine kwa kusikia, wengine kwa kugusa na wengine kwa kunusa na kuonja. Eleza hasara zisizopungua tano za kutotumia zana jumuishi.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Tano

# Mazingira ya malezi, ufundishaji na ujifunzaji katika elimu jumuishi

## Utangulizi

*Mazingira jumuishi humsaidia mwanafunzi kujifunza kikamilifu akiwa na vifaa na zana stahiki za ujifunzaji ikihusisha upatikanaji wa huduma muhimu ndani na nje ya shule. Katika sura hii utajifunza dhana ya mazingira jumuishi ya ufundishaji na ujifunzaji, mbinu za uboreshaji wa mazingira jumuishi , mbinu za uboreshaji wa malezi kwenye darasa jumuishi, na changamoto katika kutumia mbinu za kufundisha darasa jumuishi. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuboresha mazingira ya malezi, ufundishaji na ujifunzaji.*

## Fikiri

**Mazingira jumuishi yanaimarisha uhusiano kati ya mwalimu na mwanafunzi**

### Dhana ya mazingira jumuishi ya ujifunzaji

Mazingira jumuishi yanahusisha darasa lenye mazingira rafiki yanayochochea utayari wa kila mwanafunzi kujifunza kikamilifu. Mazingira haya ni pamoja na mazingira ya utendaji ya ndani na nje ya darasa yanayomwezesha mwanafunzi kujenga utayari wa kujifunza. Hii itahusisha kuwepo kwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia ambavyo vinagusa mahitaji ya kila mwanafunzi darasani ikiwemo miundombinu rafiki, mazingira safi na salama na upatikanaji wa huduma stahiki. Vilevile, uwepo wa ushirikiano kati ya mwanafunzi na mwanafunzi, mwalimu na mwanafunzi, mwalimu na mzazi/mlezi katika maendeleo ya ujifunzaji. Hivyo, mazingira jumuishi yanaweza kuwa na mifumo inayowezesha kufanya tathmini ya maendeleo ya mwanafunzi na kutoa mrejesho unaoendana na mahitaji yake.

### Sifa za mazingira jumuishi ya ujifunzaji

Mazingira jumuishi yanasifa ambazo hukuza ari ya mwanafunzi kujifunza. Mazingira hayo huhusisha:

(a) Kuwezesha upatikanaji wa mahitaji ya kila mwanafunzi nje na ndani ya darasa;

(b) Kuwepo kwa mazingira safi na salama kwa mwanafunzi kujifunza;

FOR ONLINE READING ONLY

(c) Kuwa na miundombinu rafiki na fikivu kwa kila mwanafunzi;

(d) Kuchochea uhusiano na ushirikiano mzuri kati ya mwanafunzi na mwanafunzi, mwalimu na mwanafunzi, mwalimu na mzazi/mlezi;

(e) Kuwepo kwa mbinu shirikishi na jumuishi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji;

(f) Kuwepo kwa zana jumuishi za kufundishia na kujifunzia; na

(g) Kuwepo kwa taarifa ya tathmini na mrejesho wa maendeleo ya mwanafunzi.

### Umuhimu wa mazingira jumuishi ya ujifunzaji

Mazingira jumuishi ni muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji kama ifuatavyo:

*(a)* *Kuongeza ufanisi katika ujifunzaji:* Hii inajumuisha vifaa, mbinu na rasilimali zinazosaidia katika kuelewa kwa urahisi. Mbinu na vifaa vitasaidia mwanafunzi kupata maarifa, ujuzi na kuleta matokeo chanya katika ujifunzaji;

*(b)* *Kukuza ushawishi na ushirikiano:* Ushirikiano kati ya mwanafunzi na mwanafunzi, mwanafunzi na mwalimu katika mazungumzo, majadiliano na shughuli za pamoja. Hii, humsaidia mwanafunzi kujifunza kutoka kwa wenzake au mwalimu, na anapata fursa ya kufanya kazi katika kundi na kupata maarifa tofauti yatakayoboresha ujifunzaji;

*(c)* *Kujenga ujuzi na ubunifu:* Mazingira jumuishi yanatoa fursa kwa mwanafunzi kukuza ujuzi wa vitendo kupitia stadi za kazi, michezo, na matumizi ya teknolojia. Hii itamsaidia mwanafunzi kupata ujuzi wa kiutendaji kama kufuma vitambaa, kusuka mikeka, kutengeneza vitu kama viti, vitanda na meza ambavyo ni muhimu katika soko la ajira kwa maisha ya kila siku;

*(d)* *Kuchochea hamasa ya kujifunza:* Husaidia kukuza ari na hamasa kwa mwanafunzi kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kujifunza kwa sababu mazingira yanavutia na kuhamasisha;

*(e)* *Kuimarisha maadili na nidhamu:* Mazingira jumuishi yanaimarisha maadili na nidhamu kwa mwanafunzi kwa kuwa yanahusisha sheria na kanuni zinazomwongoza katika mchakato wa kujifunza. Mfano kutopiga kelele darasani, kuhudhuria vipindi vyote kila siku, kuuliza maswali kwa utaratibu anapokuwa na changamoto na kuheshimu mawazo ya wengine darasani; na

*(f)* *Kumudu matumizi ya teknolojia:* Mazingira jumuishi humwezesha mwanafunzi kutumia programu za kielimu, vifaa saidizi, na maudhui ya ujifunzaji. Hii ni muhimu katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanakuwa na fursa sawa katika ujifunzaji.

FOR ONLINE READING ONLY

### Kazi ya kufanya 5.1

Umechaguliwa kuwakilisha chuo chako katika kongamano la kielimu, na umepewa nafasi ya kuzungumzia mazingira jumuishi ya ujifunzaji. Andaa hotuba utakayoiwasilisha ikionesha umuhimu wa mazingira jumuishi katika ufundishaji na ujifunzaji. Tumia maktaba, na vyanzo rasmi mtandaoni kupata maarifa.

### Zoezi la 5.1

1. Mazingira safi na salama ni mojawapo ya sifa katika shule jumuishi. Kwa kutumia mazingira ya chuo chako eleza namna utakavyohakikisha mazingira ya ujifunzaji ni changamshi na salama.
2. Elimu jumuishi inasisitiza ushirikishwaji wa mwanafunzi ndani na nje ya darasa. Eleza jinsi utakavyomsaidia mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo kuweza kutembea shuleni bila kikwazo chochote.

## Mbinu za uboreshaji wa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji

Mbinu za kuboresha mazingira jumuishi ya ufundishaji ni muhimu katika kuhakikisha kuwa mwalimu anafundisha kwa ufanisi na mwanafunzi anapata elimu bora. Pia, ni mchakato unaolenga kuboresha mbinu zinazochangia ufundishaji wa aina mbalimbali kulingana na mitindo tofauti ya ujifunzaji. Zifuatazo ni mbinu za uboreshaji wa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji:

(a) *Kuboresha miundombinu ya shule:* Kuwa na madarasa yenye nafasi, mwanga wa kutosha, na hewa safi. Kuwepo kwa samani za darasa zinazobadilika kulingana na mahitaji ya mwanafunzi. Vilevile, kuwa na uwekezaji wa vifaa vya TEHAMA ikihusisha matumizi ya vifaa vya teknolojia kama vile projekta, kompyuta zenye programu saidizi na vinasa sauti. Hii inaweza kusaidia mwanafunzi na mwalimu kupata rejea mbalimbali za masomo mtandaoni;

(b) *Kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji:* Kuwa na mbinu zinazomshirikisha mwanafunzi kama vile, kujifunza katika jozi, majadiliano ya vikundi, na maonesho ya vitendo. Hii inachochea ufahamu wa kina na ushirikiano wa mwanafunzi katika ujifunzaji. Vilevile, kutumia mafunzo kwa vitendo, kazimradi, na ziara za kielimu ili kumsaidia mwanafunzi kuelewa dhana kwa njia ya vitendo;

(c) *Kutekeleza mafunzo endelevu ya walimu kazini:* Walimu kuwa na mafunzo ya mara kwa mara kuhusu mbinu mpya za ufundishaji, usimamizi wa darasa, uchopekaji wa masuala mtambuka na matumizi ya teknolojia. Mafunzo haya

FOR ONLINE READING ONLY

yanaweza kuwa ya kitaaluma na kitaalamu yatakayowezesha kujenga umahiri na ujuzi uliokusudiwa. Vilevile, ni muhimu kuanzisha Jumuiya za Kujifunza (JzK) ambazo zitajumuisha timu za walimu kwa ajili ya kubadilishana mawazo, kupanga shughuli za masomo, na kutatua changamoto za ufundishaji kwa pamoja;

(d) *Kutekeleza ushirikiano wa wazazi/walezi/jamii na walimu shuleni:* Ushirikiano huu, utaboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kuwa salama kwa ajili ya malezi, makuzi na ujifunzaji wenye ufanisi. Aidha, itasaidia kuimarisha mawasiliano, uwazi, usawa wa kijinsia na uwajibikaji kati ya shule na jamii kwa ujumla. Wazazi, kwa kushirikiana na walimu, wanaweza kuunda timu jumuishi itakayoratibu ushirikiano huo ndani na nje ya shule; na

(e) *Kufanya ufuatiliaji na tathmini:* Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ili kufanya utambuzi wa mapema na kubaini changamoto ili kutoa afua stahiki. Hii itahusisha matumizi ya mbinu na zana za upimaji katika ubainishaji wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kama vile uchunguzi, majadiliano, hojaji, historia ya afya ya mwanafunzi na kutumia orodha hakiki. Hivyo, ni muhimu kutumia tathmini za mara kwa mara ili kupima ufanisi wa mbinu na zana za ufundishaji, mazingira ya ujifunzaji, na kufanya maboresho yanayohitajika.

### Kazi ya kufanya 5.2

Utekelezaji wa mikakati ya elimu jumuishi huhitaji mbinu za uboreshaji wa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Eleza mbinu zitakazowezesha kutumika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika darasa jumuishi. Andika dondoo na hifadhi katika mkoba wa kazi

### Zoezi la 5.2

1. Ukiwa kama mtaalamu wa elimu jumuishi, eleza maeneo yanayozingatiwa katika uboreshaji wa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.
2. Eleza mchango wa jamii katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwenye shule jumuishi.

## Mbinu za uboreshaji wa mazingira ya malezi kwenye darasa jumuishi

Malezi ni mchakato wa kumlea, kumtunza na kumwongoza mwanafunzi ili aweze kukua na kuendelezwa kimwili, kiakili, kijamii na kihisia. Malezi yanahusisha kutoa

FOR ONLINE READING ONLY

mafunzo, msaada na mazingira salama ambayo yanamwezesha mwanafunzi kupata stadi muhimu za maisha. Programu ya Malezi Jumuishi kwa Tanzania Bara ya Mwaka 2022, imesisitiza kuwa na malezi jumuishi katika kutoa huduma za malezi stahiki kwa watoto na wanafunzi wote. Hivyo, mchakato wa malezi unaweza kufanywa na mzazi, mlezi, mwalimu, na wadau wengine waliopo karibu na mwanafunzi.

Aidha, kuboresha malezi katika darasa jumuishi ni muhimu ili kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi, bila kujali tofauti zilizopo, anapata nafasi sawa ya kujifunza na kukua katika mazingira ya kuheshimiana, kutambulika na kushirikiana. Zifuatazo ni mbinu za kuboresha mazingira ya malezi katika darasa jumuishi:

(a) *Kutoa huduma na afua stahiki katika malezi:* Kutoa huduma za kibinafsi kulingana na mahitaji ya kila mwanafunzi;

(b) *Kutumia mikakati inayozingatia mahitaji ya kila mwanafunzi:* Kuwa na mbinu mbalimbali za kufundishia kama vile majadiliano katika vikundi, mafunzo ya vitendo, michezo, nyimbo na masimulizi ili kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anapata fursa ya kujifunza kulingana na mitindo ya ujifunzaji. Aidha, mwanafunzi ahusishwe katika kila hatua ya ujifunzaji. Hii ni pamoja na kumshirikisha kila mwanafunzi katika shughuli za darasani kwa kumpa fursa sawa ya kutoa maoni, na kuuliza maswali;

(c) *Kuandaa mazingira salama na jumuishi:* Kuandaa mazingira rafiki ya darasa kuwa mahali salama na penye msaada, ambapo kila mwanafunzi atajisikia kupendwa na kuthaminiwa. Hii inaweza kuhusisha kutengeneza kanuni na taratibu za darasa zinazosisitiza usalama na uwajibikaji wa kila mwanafunzi ili kuondoa ubaguzi na udhalilishaji ndani na nje ya darasa; na

(d) *Kutathmini ufanisi wa mbinu za malezi:* Kufanya tathmini ya mara kwa mara ya mbinu za malezi zinazotumika darasani ili kuhakikisha ujumuishi wa kila mwanafunzi. Aidha, maboresho ya mazingira ya malezi kwenye darasa jumuishi, yanaweza kufanywa kupitia matokeo ya tathmini hizi.

Mbinu hizi zinaweza kuboresha malezi katika madarasa jumuishi, hivyo kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anajisikia kukubalika, kupata elimu bora, na kuendelea vyema kiakili, kimwili, kihisia na kijamii.

FOR ONLINE READING ONLY

## Kazi ya kufanya 5.3

Tumia vyanzo rasmi mtandaoni kutazama video kuhusu mbinu za uboreshaji wa mazingira ya malezi kwenye darasa jumuishi zinavyochangia ujifunzaji. Kwa kutumia video uliyotazama. Eleza mbinu zitakazo kusaidia kuboresha mazingira ya malezi katika shule jumuishi nchini Tanzania. Hifadhi ripoti kwenye mkoba wa kazi.

## Zoezi la 5.3

1. Elimu jumuishi shuleni inazingatia malezi, makuzi na maendeleo ya mwanafunzi katika kujifunza kwa ufanisi. Eleza namna mbinu za kuboresha mazingira ya malezi zinavyoweza kumjengea mwanafunzi kumudu stadi za karne ya 21.
2. Mazingira jumuishi huhusisha wanafunzi wenye ulemavu na wasio na ulemavu. Eleza mbinu za uboreshaji wa mazingira ya malezi utakazozitumia kumsaidia mwanafunzi mwenye changamoto ya kihisia na kitabia.

## Changamoto katika kutumia mbinu za uboreshaji wa mazingira ya malezi katika darasa jumuishi

Uboreshaji wa mazingira ya malezi katika darasa jumuishi ni muhimu kwani inampa fursa mwalimu kufanya tathmini na kuandaa mazingira jumuishi kwa mwanafunzi kushiriki, kujifunza na kuchangamana na mazingira hayo. Pamoja na mbinu hizi, kuna changamoto ambazo ni vikwazo katika utekelezaji wa uboreshaji huo:

(a) Upatikanaji wa rasilimali: Madarasa jumuishi yanahitaji vifaa maalumu kama vile teknolojia na vifaa saidizi vya kumsaidia mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kujifunza. Hata hivyo, shule nyingi zinaweza kukosa bajeti ya kununua vifaa hivi, na hivyo kumfanya mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kukosa msaada unaofaa. Hivyo ni muhimu upatikanaji wa rasilimali ukazingatiwa ikiwemo teknolojia na vifaa saidizi;

(b) Ukosefu wa mafunzo ya walimu: Mwalimu anaefundisha katika darasa jumuishi anahitaji ujuzi maalumu ili aweze kushughulikia mahitaji tofauti na namna ya kutoa afua stahiki kwa kila mwanafunzi. Aidha, baadhi ya walimu hawapati mafunzo ya kutosha kuhusu jinsi ya kufundisha na kusimamia darasa jumuishi, na hii inaweza kuathiri ubora wa malezi na elimu wanayotoa. Kwa hiyo, ni muhimu walimu wapatiwe mafunzo ya kumudu usimamizi na malezi katika darasa jumuishi;

(c) Utofauti wa mahitaji ya wanafunzi: Mwanafunzi anaweza kuwa na mahitaji na uwezo tofauti katika ujifunzaji. Hivyo, mwalimu anaweza asiwe na mbinu za kusimamia tofauti hizi na kutoa huduma stahiki. Mwalimu anapaswa kutumia elimu ya utambuzi ili kubaini changamoto zinazojitokeza darasani;

(d) Mitazamo hasi ya wazazi/walezi na jamii: Baadhi ya wazazi/walezi wanaweza kuwa na mtazamo hasi kuhusu elimu jumuishi, wakihisi kwamba watoto wao watakosa msaada wa kutosha au watashuka kiwango cha ujifunzaji. Hii inaweza kusababisha migogoro kati ya walimu na wazazi, na kuathiri utekelezaji wa mbinu za kuboresha malezi. Hivyo wazazi waelimishwe kuhusu elimu jumuishi; na

FOR ONLINE READING ONLY

Zoezi la 5.3

1. Elimu jumuishi shuleni inazingatia malezi, makuzi na maendeleo ya mwanafunzi katika kujifunza kwa ufanisi. Eleza namna mbinu za kuboresha mazingira ya malezi zinavyoweza kumjengea mwanafunzi kumudu stadi za karne ya 21.
2. Mazingira jumuishi huhusisha wanafunzi wenye ulemavu na wasio na ulemavu. Eleza mbinu za uboreshaji wa mazingira ya malezi utakazozitumia kumsaidia mwanafunzi mwenye changamoto ya kihisia na kitabia.

## Changamoto katika kutumia mbinu za uboreshaji wa mazingira ya malezi katika darasa jumuishi

Uboreshaji wa mazingira ya malezi katika darasa jumuishi ni muhimu kwani inampa fursa mwalimu kufanya tathmini na kuandaa mazingira jumuishi kwa mwanafunzi kushiriki, kujifunza na kuchangamana na mazingira hayo. Pamoja na mbinu hizi, kuna changamoto ambazo ni vikwazo katika utekelezaji wa uboreshaji huo:

(a) Upatikanaji wa rasilimali: Madarasa jumuishi yanahitaji vifaa maalumu kama vile teknolojia na vifaa saidizi vya kumsaidia mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kujifunza. Hata hivyo, shule nyingi zinaweza kukosa bajeti ya kununua vifaa hivi, na hivyo kumfanya mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kukosa msaada unaofaa. Hivyo ni muhimu upatikanaji wa rasilimali ukazingatiwa ikiwemo teknolojia na vifaa saidizi;

(b) Ukosefu wa mafunzo ya walimu: Mwalimu anaefundisha katika darasa jumuishi anahitaji ujuzi maalumu ili aweze kushughulikia mahitaji tofauti na namna ya kutoa afua stahiki kwa kila mwanafunzi. Aidha, baadhi ya walimu hawapati mafunzo ya kutosha kuhusu jinsi ya kufundisha na kusimamia darasa jumuishi, na hii inaweza kuathiri ubora wa malezi na elimu wanayotoa. Kwa hiyo, ni muhimu walimu wapatiwe mafunzo ya kumudu usimamizi na malezi katika darasa jumuishi;

(c) Utofauti wa mahitaji ya wanafunzi: Mwanafunzi anaweza kuwa na mahitaji na uwezo tofauti katika ujifunzaji. Hivyo, mwalimu anaweza asiwe na mbinu za kusimamia tofauti hizi na kutoa huduma stahiki. Mwalimu anapaswa kutumia elimu ya utambuzi ili kubaini changamoto zinazojitokeza darasani;

(d) Mitazamo hasi ya wazazi/walezi na jamii: Baadhi ya wazazi/walezi wanaweza kuwa na mtazamo hasi kuhusu elimu jumuishi, wakihisi kwamba watoto wao watakosa msaada wa kutosha au watashuka kiwango cha ujifunzaji. Hii inaweza kusababisha migogoro kati ya walimu na wazazi, na kuathiri utekelezaji wa mbinu za kuboresha malezi. Hivyo wazazi waelimishwe kuhusu elimu jumuishi; na

FOR ONLINE READING ONLY

(e) *Upungufu wa wataalamu:* **Baadhi ya shule zinakabiliwa na upungufu wa wataalamu wa elimu maalumu kama vile wanasaikolojia, wataalamu wa lugha ya alama, na wataalamu wa viungo. Hii inaweza kusababisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu asipate msaada unaohitajika kwa wakati. Hivyo, ni muhimu kuwa na wataalamu wa elimu maalumu ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.**

## Kazi ya kufanya 5.4

**Uwekezaji katika ufundishaji na ujifunzaji unategemea rasilimali fedha, muda na watu. Tembelea idara ya ualimu chuoni, fanya mahojiano na uongozi wa idara hiyo kuhusu changamoto za upatikanaji wa rasilimali hizo kwenye somo la elimu jumuishi na namna wanavyozitatua. Andika nukuu na hifadhi katika mkoba wa kazi.**

## Zoezi la marudio

1. **Serikali imetilia mkazo kuhusu elimu jumuishi shuleni, lakini utekelezaji wake ni mdogo kutokana na mtazamo hasi wa jamii. Eleza jinsi utakavyosaidia kutatua changamoto hiyo.**
2. **Elimu jumuishi inasisitiza ushirikishwaji wa mwanafunzi katika ujifunzaji ndani na nje ya darasa. Eleza jinsi utakavyomsaidia mwanafunzi anayetumia kiti mwendo kutembea shuleni bila vikwazo vyovyote.**
3. **Kama mwalimu mkuu, umepewa shule yenye changamoto ya miundombinu isiyo rafiki katika ujifunzaji. Eleza utakavyoboresha miundombinu ya shule ili kusaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu kupata elimu kwa ufanisi.**
4. **Chambua changamoto utakazoziwasilisha katika Jumuiya za Kujifunza (JzK) kwa ajili ya kuboresha mazingira ya malezi shuleni kwako.**

FOR ONLINE READING ONLY

# Misamiati

| | |
|---|---|
| Afasia | Changamoto inayoatthiri uwezo wa kuwasiliana (kutafsiri na utamkaji) |
| Afua | Hatua zinazochukuliwa kusahihisha, kurekebisha au kuzuia na kutambua tiba zinazowezekana |
| Afua stahiki | Hatua, mchakato au mikakati inayochukuliwa kwa uangalifu na ujuzi ili kuhakikisha kuwa changamoto za mwanafunzi ndani na nje ya darasa zinatatuliwa kwa ubora |
| Apraksia | Changamoto ya utendaji unaosababishwa na kuumizwa ubongo kutokana na ajali, kiharusi, na/au magonjwa ya neva |
| Disathria | Changamoto ya utamkaji wa maneno mfano kuwa na kithembe au kigugumizi |
| **Disgrapfia** | Changamoto wakati wa uandishi na kuchanganya herufi mfano m/w |
| Diskalkulia | Changamoto wakati wa kuhesabu, kukokotoa, uandishi wa namba, utambuzi wa namba na kupanga namba |
| Disleksia | Changamoto wakati wa kusoma kwa mfano kuchanganya herufi "m" na "w", "i" na "l", "n" na "u", "b na "d". |
| Elimu jumuishi | Elimu inayotolewa kwa watu wote bila kujali tofauti zao ikiwemo umri, jinsi, utamaduni, uchumi, maumbile, hali, ulemavu na uwezo katika ujifunzaji |
| Jumuiya za Kujifunza | Jumuiya ambazo zinahusisha kundi la walimu kukaa pamoja na mwezeshaji kufanya majadiliano ya shughuli zinazolenga kuboresha ujifunzaji |
| Kabrasha | Sehemu ya kuhifadhia majalada yenye kazi mbalimbali |
| Kusinyaa kwa misuli | Kulegea na kutofanya kazi kwa misuli |
| Makunzi | Malighafi zinazotumika katika kutengenezea zana mfano, kasha, uzi, mbegu, mchanga, karatasi, unga na vijiti |

FOR ONLINE READING ONLY

| | |
|---|---|
| Maliwato | Neno la Kiswahili linalotumika kumaanisha choo |
| Mashine ya Braille | Kifaa kinachotumika kuandika maandishi yanayosomwa na wasioona |
| Mchakato | Hatua za kutenda/kufuata ili kufikia lengo/jambo fulani |
| Mgongo wazi | Ulemavu wa kuwa na tobo kwenye uti wa mgongo |
| Mkoba wa kazi | Kusanyiko la kazi maalumu zilizochaguliwa na kuhifadhiwa na wanafunzi katika jalada au bahasha kubwa |
| Shime sikio | Ni kifaa kinachotumika kukuza mawimbi ya sauti |
| Ufaraguzi | Kitendo cha kugeuza matumizi halisi ya kifaa husika na kukifanya kuwa zana ya kufundishia na kujifunzia |
| Ulemavu | Hali ya kuwa na hitilafu ya kudumu au ya muda mfupi mwilini au akilini inayomzuia mtu kutekeleza shughuli au majukumu ya kawaida katika Maisha ya jamii |
| Usonji | Ni hali ya neva za fahamu kushindwa kufanya kazi vizuri hivyo kupelekea kukosa mawasiliano, utambuzi na kushirikiana na wengine |

FOR ONLINE READING ONLY